SportPesa
TZS. 1,065,872,000
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Nyati** aua watu watatu wakiwa shambani
UKURASA 2




**ORIGI KUTIMKA LIVERPOOL**
UKURASA 21

Nipashe
Ijumaa Machi 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580895
www.ippmedia.com
The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

RIPOTI MAALUM

# Uchafuzi wa Mto Mara unavyotesa wananchi

UKURASA 4



Mwenyekiti wa Kitongoji cha Burongo, Kijiji cha Bisarwi wilayani Tarime, Juma Matinde (kushoto), akifafanua jambo kwa maofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), walipotembelea moja ya maeneo yaliyodhurika kutokana na uchafuzi wa Mto Mara hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**SAMIA: TUNASAKA FEDHA ZA UJENZI WA BARABARA**
RAIS Samia Suluhu Hassan amezindua mradi wa daraja la Tanzanite jijini...

UKURASA WA 3
**MFUMO WAJA KUKABILI UHABA WA WATUMISHI**
SERIKALI imezindua mfumo wa kielektroniki wa tathmini ya hali ya watumishi...

UKURASA WA 16
**MCHAKATO RASIMU SERA YA UWEKEZAJI WAANZA**
WIZARA ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kuwatumia wataalam wa masuala...

## Serikali yataja maeneo manne uwekezaji wa sekta ya afya

UKURASA 3



## Gumzo mtandaoni Mrema kufunga ndoa kipindi cha Kwaresma

UKURASA 2

MICHEZO | SIMBA YAJIPANGA ROBO FAINALI CAF UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea mchoro wa picha ya daraja la Tanzanite kutoka kwa Balozi wa Korea Kusini hapa nchini, Kim Sun Pyo, wakati wa uzinduzi wa daraja hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Gumzo mtandaoni Mrema kufunga ndoa Kwaresma

**Na Waandishi Wetu**

GUMZO liliibuka jana katika mitandao ya kijamii kutokana na Mwenyekiti wa Tanzania Labor Party (TLP), Augustine Mrema, kufunga ndoa katika kipindi cha Kwaresma.

Ndoa ya mwanasiasa huyo mkongwe ilifungwa jana katika Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi, Parokia ya Uomboni, Kijiji cha Kiraracha.

Kwa kawaida, katika kipindi kama hiki, baadhi ya madhehebu ya Kikristo yakiwamo ya Katoliki, Kilutheri na Anglikana huwa hayafungishi ndoa ndiyo maana yakaibuka maswali kutokana na kujitokeza kwa jambo hilo.

Mrema alifunga ndoa na mwanamke mwingine kutokana na kufiwa na mke wake, Rose Mrema, Septemba, mwaka jana.

Baadhi ya watu waliohoji kuhusu ndoa hiyo kwenye mitandao ya kijamii, walikuwa na maswali mmoja akisema: "Wakatoliki wenzangu hebu nisaidieni, hivi huwa kuna ndoa kipindi cha Kwaresma? Inawezekana nachanganya mambo!"

Mwingine alijibu "Kama ni dharura wanapewa kibali ndoa inafungwa" huku mwingine akijibu hoja hiyo alisema; "ndoa zipo ila hazina shamrashamra." Mtoa maoni huyo aliyesema ni muumini wa Kanisa Katoliki alisema: "Kukiwa na sababu maalum huwa inafungwa."

Mwingine alisema: "Hakuna ndoa kipindi hiki cha Kwaresma hususan sisi Wakatoliki labda kama mzee ameomba kwa sababu maalum..."

Paroko wa Parokia ya Uomboni, Padri Adelard Imani, aliyefungisha ndoa hiyo alipoulizwa kwa nini ndoa hiyo imefungwa wakati huu wa Kwaresma, alimwambia mwandishi kwamba: "Naomba nikujibu baadaye kidogo" lakini mpaka jioni alikuwa hajafanya hivyo.

Mkurugenzi wa Mawasiliano Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Chesco Msaga, alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, alisema: "Askofu wa Jimbo ametafsiri Sheria za Kanisa Katoliki. Hadi paroko anafungisha hiyo ndoa kipindi hiki, maana yake kuna kibali cha askofu, vinginevyo asingefanya hivyo."

Mrema amefunga ndoa na mwanamke mwingine kutokana na kufiwa na mke wake, Rose Mrema, Septemba, mwaka jana.

**ASIMULIA MAGUMU**

Mrema alisema baada ya mke wake kufariki dunia Septemba mwaka jana, aliishi katika mazingira magumu, hivyo alimwomba Mungu amsaidie ili apate msaidizi mwingine.

"Baada ya mke wangu kufariki (dunia) afya ilikuwa imedorora hata hotuba yangu wakati wa kumzika sikuweza kusimama. Nilimwomba Mungu anisaidie nipate mtu atakayenitunza, atakayenialika," alisema.

Kutokana na maombi yake hayo, alisema baraka za Mwenyezi Mungu zilishuka na ndipo akajitokeza huyo binti (Doreen) akakubali kutumia maisha yake kwa ajili ya kumtunza.

"Binti huyu (mke wake) alipojitokeza aliniambia kuwa kutokana na kazi nzuri niliyoifanya mimi (Mrema) katika taifa hili, umetutumikia sisi wananchi, hivyo niko tayari kutumia maisha yangu kukuhudumia. Kwa hiyo tulitafutana tukaelewana na akakubali kwa hiari yake," alisema.

●**Imeandikwa na Mwandishi Wetu, DAR na Thobias Mwanakatwe, MOSHI**

## Watatu wauawa na nyati

**Na Abdallah Khamis,**
MTWARA

WATU watatu katika Kijiji cha Mahurunga Wilaya ya Mtwara mkoani hapo, wamefariki dunia baada ya kushambuliwa na nyati wakati wakiwa katika shughuli za kilimo kwenye mashamba yao.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi (ACP) Nicodemus Katembo, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Machi 20, mwaka huu.

Katembo aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Rashid Bakari (40) mkazi wa Kijiji cha Kitunguli, Salum Kumbemba (46) ma Said Musa (45) wote wakazi wa Kijiji cha Mahurunga.

Alisema nyati huyo alifika ghafla katika kijiji cha Mahurunga akitokea porini na kufanya shambulizi kwa watu hao waliokuwa katika shughuli za kujitafutia riziki.

"Baada ya shambulizi hilo la nyati, taarifa ziliwafikia askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wanaolinda mpaka ambao walifika haraka na kumuua mnyama huyo kabla hajaleta madhara zaidi," alisema Katembo.

Alisema baada ya uchunguzi wa miili ya marehemu kufanyika, ndugu waliruhusiwa kuichukua kwa ajili ya maziko.

Katika hatua nyingine, ACP Katembo alisema kutokana na kumsaka mwanamke aliyemtupa mtoto anayekadiriwa kuishi kwa saa nane kabla ya kufariki dunia unaendelea. Alisema mtoto huyo alitupwa Machi 22 majira ya asubuhi na mtu asiyejulikana ambapo wakazi wa mtaa wa Coco Beach, walibaini tukio hilo baada ya kusikia sauti ya mtoto akilia kutokea katika dampo la taka lililo katika eneo hilo.

MARIPELANTO COMPANY LIMITED
N.I.C LIFE HOUSE, 6th Floor WING "C"
P.O Box 7839, Sokoine Drive/Ohio Street
+255 620559506 / +255 713341077

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi MARIPELANTO COMPANY LIMITED kwa idhini iliyopewa na KCB BANK TANZANIA LIMITED P.O Box 804 Dar Es Salaam Tanzania (KCB Bank), tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara jengo la makazi na biashara linalojulikana kama ABLA APARTMENTS lililopo Mikocheni Kwa Mwalimu Nyerere kama ilivyoainishwa hapa chini

| S/N | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | ABLA ESTATES DEVELOPERS & AGENCY COMPANY LIMITED | **Nyumba za Makazi/Biashara (ABLA APPARTMENTS)** Kitalu No. 489, Hati ya kiwanja No.30063 Eneo la Mikocheni B, **Kwa Mwalimu Nyerere**, Manispaa ya Kinondoni | 16/04/2022 |

1. Dhamana itauzwa kwa mnunuzi aliyetoa dau kubwa kuliko wengine lakini Bank ina haki ya kukubali au kukataa mauzo hayo bila kutoa sababu yeyote.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki 75% kilipwe ndani ya siku 14 au ndani ya muda utakaowekwa kwa makubaliano kati ya Bank na Mnunuzi.
3. Mnunuzi akishindwa kumalizia 75% ya malipo yaliyobaki, fedha aliyotoa haitarudishwa na mali itarudishwa kuuzwa katika mnada mwingine siku itakayotangazwa.
4. Gharama za kubadilisha hati miliki na gharama nyinginezo ni za mnunuzi
5. Dhamana zitauzwa kama zilivyo
6. Ukaguzi wa dhamana utafanyika tatu (3) kabla ya siku ya Mnada kuanzia saa4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni

KWA MAWASILIANO ZAIDI

MKURUGENZI MTENDAJI,
MARIPELANTO COMPANY LIMITED
NIC LIFE HOUSE
P.O BOX 7837 DSM
SIMU 0762610537

KCB BANK HQ
AFISA MIKOPO
HARAMBEE PLAZA
P.O BOX 804 DSM
SIMU 0755379787/0767210578

# Samia: Tunasaka fedha ujenzi wa barabara

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amezindua mradi wa daraja la Tanzanite jijini Dar es Salaam, na kueleza kuwa serikali inatafuta fedha za kutosha kwa ajili ya barabara vijijini na mijini.

Alitoa kauli hiyo jana katika uzinduzi huo wa daraja lililojengwa kwa fedha za mkopo nafuu kutoka serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini wa Dola za Marekani milioni 123.032 na serikali ikitoa Dola milioni 4.233 kwenye kodi na gharama stahili za uendeshaji mradi.

Rais Samia alisema uzinduzi wa daraja hilo lenye urefu wa kilometa 1.03 na barabara unganishi yenye urefu wa kilometa 5.2, ni sehemu ya kumuenzi Hayati Rais John Magufuli.

"Tunatafuta fedha za kutosha kwa ajili ya barabara za vijijini na mijini zinazosimamiwa na TARURA (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) chini ya Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)," alisema.

Alikumbusha kuwa ujenzi wa barabara na madaraja una gharimu fedha nyingi, na kuwa lazima zitunzwe na kuitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ihakikishe miundombinu hiyo inafanyiwa matengenezo stahiki kwa muda mwafaka.

"Serikali tutafanya jitihada za kutosha za matengenezo ya barabara zote nchi nzima kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) inayosimamia barabara kuu na barabara za mikoa na barabara za mijini chini ya wizara hii," alisema.

Alisema ujenzi wa daraja ni mwendelezo wa kuboresha miundombinu ili kukabiliana na kero ya msongamano wa magari ikiwamo kuzipanua na kuzijenga za mlisho, madaraja ya juu na za mabasi yaendayo haraka.

Alisema kwa sasa ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka unaendelea ambapo awamu ya tatu itahusisha barabara kutoka katikati ya jiji kwenda Gongo la Mboto. "Awamu ya nne kutoka katikati ya jiji kwenda Tegeta, awamu ya tano kutoka Ubungo hadi bandarini hadi Nelson Mandela, kutoka Kigogo kwenda Tabata Dampo hadi Segerea na awamu ya sita kutoka Morocco kwenda Kawe hadi Lugalo," alisema.

Rais Samia alisema miradi yote ikikamilika itaondoa msongamano wa magari mkoani Dar es Salaam na kuongeza kwa kiasi kikubwa ukuaji wa shughuli za uchumi na biashara na itaongeza muda wa watu kufanya kazi. Pia alisema itapunguza gharama za mafuta yanayotumiwa na vyombo vya usafiri na migogoro majumbani kwa watu kuchelewa kurudi kwa visingizio vya foleni.

Alisema miradi yote ikikamilika itabadili madhari ya jiji la Dar es Salaam kwa kulipendezesha huku akitolea mfano daraja hilo la Tanzanite waenda kwa miguu nyakati za jioni wanaweza kulitumia kuangalia ufukwe wa Bahari ya Hindi.

Alibainisha kuwa jitihada kama hizo pia zinaendelea kwenye miji na majiji mengine likiwamo jiji la Dodoma ambapo karibuni aliweka jiwe la msingi kwa ajili ya barabara ya mzunguko.

Akizungumzia jina la daraja hilo alisema amepokea ushauri wa wananchi ambao wanataka iwekwe alama ya tanzanite kuliko ya Mwenge iliyopo sasa ili kukamilisha jina lake.

HABARI KITAIFA

# Serikali yataja maeneo manne uwekezaji afya

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imewaita wawekezaji kutoka India na nchi zingine duniani kuwekeza katika sekta ya afya kwenye maeneo manne makubwa, ikiwamo ujenzi wa hospitali za kutoa huduma za kibingwa kwenye mikoa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alieleza kuhusu mpango huo mkoani Dar es Salaam wakati wa mkutano uliokutanisha wadau wa Tanzania na India kuangalia fursa za uwekezaji nchini katika sekta ya afya. Mkutano huo uliandaliwa na Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan.

Akifungua mkutano huo, Prof. Makubi alisema wanawashawishi wawekezaji kuwekeza katika utoaji wa huduma za kibingwa na bobezi kwa sababu kwa sasa nyingi zinapatikana Dar es Salaam.

"Tunataka ziende kwenye mikoa. Tunaweza kuwekeza kwa pamoja na wawekezaji au wakawekeza wao kwa asilimia 100," alisema.

Eneo la pili ni kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba kwa kuwa hadi sasa vilivyopo havifiki 10 na vingi vinatengeneza dawa chache ambazo hazizidi asilimia tano ya mahitaji yaliyopo.

"Asilimia 95 ya dawa na vifaa tiba tunategemea kuagiza kutoka nje. Tunawaita wawekezaji waje kuwekeza katika eneo hilo ikiwamo viwanda vya kuzalisha chanjo," alisema. Alitaja eneo la tatu ni uchunguzi wa kisasa kwa sababu wananchi wanapougua hutaka huduma kwa haraka.

Prof. Makubi alitaja la mwisho ni mafunzo ambapo wawekezaji wanaweza kuwekeza kwa kujenga vyuo ili kuwezesha huduma hiyo kupatikana badala ya wataalamu kwenda nje kuitafuta.

Kuhusu ushirikiano kati ya India na Tanzania, Prof. Makubi alisema nchi hizo zimeshirikiana zaidi ya miaka 50 katika sekta mbalimbali ikiwamo afya.

"India imewekeza katika mafunzo tumekuwa tukiwapeleka India wataalam wetu wa afya kwa ajili ya mafunzo zaidi. Katika udaktari bingwa bobezi India walitusaidia kutoa mafunzo kwa wataalam zaidi ya 20 ambao baada ya kurejea ndipo ilipoanzishwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)," alisema.

"Tunashirikiana nao katika sekta ya upasuaji mbalimbali, kufanya kambi hapa nchini za ugunduzi wa magonjwa mbalimbali," aliongeza.

Balozi Pradhan alisema wanazihamaisha hospitali zinazoongoza India kuja Tanzania kuwekeza kwa sababu hadi sasa nyingi zinatoa huduma za kawaida katika mikoa tofauti nchini.

Alisema kila mwaka ubalozi wao umekuwa ukitoa Visa 2,500 kwa watanzania wanaokwenda nchini India kupata matibabu.

# Mfumo rasmi kukabili uhaba watumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua mfumo wa kielektroniki wa tathmini ya hali ya watumishi katika utumishi wa umma unaolenga kubaini mahitaji halisi ya watumishi kwenye wizara na taasisi za umma.

Hata hivyo, tathmini iliyopo imebainisha kuwa utoshelevu wa mahitaji ya watumishi kwa taasisi za umma upo kati ya asilimia 52 hadi 90.

Akizindua mfumo huo jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema mfumo huo unalenga kujua idadi, majukumu yao na vituo wanavyofanyia kazi.

Alisema mfumo huo utasaidia kutathmini hali halisi ya watumishi walioko na wanaohitajika katika taasisi zote za umma ili kuwapanga kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kila taasisi.

"Kwa kufanya hivyo, serikali itakuwa na taarifa na takwimu sahihi kuhusu watumishi waliopo, mahitaji ya watumishi wanaohitajika katika kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi," alisema.

Aidha, alisema matarajio ni kuweka msawazisho wa watumishi wa umma katika taasisi za umma.

"Kwa tathmini iliyoko inabainisha kuwa utoshelevu wa mahitaji ya watumishi kwa taasisi za umma upo kati ya asilimia 52 hadi 90, zipo baadhi ya taasisi ambazo zina watumishi wa ziada katika baadhi ya kada," alisema.

Alifafanua kuwa tathmini hiyo ilianza Januari mwaka huu na ililitakiwa likamilike katikati ya Februari, 2022, na hadi sasa inaonyesha bado wizara na taasisi nyingi hazijakamilisha.

"Kwa taarifa tulizo nazo mpaka leo kati ya wizara na taasisi 427 zilizo kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara katika Utumishi wa Umma (HCMIS) zote zimeshaanza kutumia mfumo na zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa zoezi hili na zipo kati ya asilimia 13 hadi 97."

Alisema bado kuna wizara na taasisi nyingi hazijatekeleza maelekezo ya serikali ipasavyo.




International School of Tanganyika
Challenge | Support | Inspire

PO Box 2651 Dar es Salaam, Tanzania
Central and Elementary Office Phone: +255 684 228882/3 +255 658 228883/5
Secondary Office Phone: +255 22 260 1126/7 or +255 787 997778/98
Web: www.istafrica.com
Email: information@istafrica.com

## INVITATION FOR BIDS

Bids are invited from interested registered, competent, reliable and licensed suppliers/dealers to provide the under listed goods and services for the year ending 31st July 2023.

| S/N | Category No. | Description |
|---|---|---|
| 1. | Category 01 | Maintenance Materials |
| 2. | Category 02 | Consumables and Cleaning Materials |
| 3. | Category 03 | Office Stationery |
| 4. | Category 04 | Staff Welfare Supplies (Sugar, Tea, Coffee & Milk Powder) |
| 5. | Category 05 | Timber |
| 6. | Category 06 | Supply and Servicing of Fire Extinguishers |
| 7. | Category 07 | Fumigation |
| 8. | Category 08 | Cesspit Emptying |
| 9. | Category 09 | Appliances (Fridges, Cookers & Air-conditions) |
| 10. | Category 10 | Motor Vehicle Spare Parts |
| 11. | Category 11 | Service of Equipment |

**Conditions:**

- Bid document(s) will be emailed to the bidders on payment of TZS. 50,000/= payable per bid category. Payments should be made to the Billing Department located in the Administration Building (Gate #5), off United Nations Road, Upanga, between 10.00 am to 1.00 pm Monday to Friday. Bidders will need to provide the School with the email ID at the time of making payment. Once payment has been received, bid documents will be emailed by the following working day.
- Bids should be emailed to bids@istafrica.com latest by 2 p.m. on Thursday, April 14, 2022. No bids will be accepted after this time. In addition, bidders should attach scanned copies of certificates of registration, business license, TIN/VAT certificates and User Identification Number certificate (for VAT registered suppliers). On submission of the information, the bidders would receive a confirmation that their bids have been successfully received by IST.
- The School is not bound to accept the lowest or any bid and reserves the right to reject all or any of the bids received.

CIS WE ARE AN ACCREDITED SCHOOL

RIPOTI MAALUM

# Uchafuzi wa Mto Mara unavyowatesa wakazi

● MAGONJWA YASIYOELEWEKA, MIFUGO NA SAMAKI WAFA



Sehemu ya Mto Mara wilayani Tarime ambayo mwanzoni mwa mwezi huu maji yake yalichafuliwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

INAPOTOKEA mtu anasogea hadi Kata ya Manga wilayani Tarime na kuzuru kwenye vijiji vyake kama vile Bisarwi na Kembwi, mara moja ushuhuda wake utagundua kuna kitu kisicho cha kawaida katika afya. Ndiyo dodosa zilizoifikia Nipashe ilipofika mahali hapo.

Ni msamiati wa utani, lakini ndiyo umebeba ukweli kuwapo ugonjwa unaoitwa 'kwangua vocha' kwa maana kuna nyakati baadhi ya wanavijiji wanashuhudiwa wakijikuna mithili ya tendo hilo, hali kadhalika kukohoa.

Pia, inaendana na suala la kuhara na kutapika linalokuwa la kawaida, tumbo kuvimba na madhila mengine ya jamii hiyo. Ni kwa bahati mbaya, hitaji la huduma za afya iwe zahanati au kituo cha afya kwa wanaopatwa na madhila hayo ni sharti kufunga safari wastani wa kilomita nne wakahudumiwe.

Uchunguzi wa Nipashe kwenye eneo hilo, uliopewa uthibitisho kutoka kwa wenyeji wanavijiji, umebaini kuwapo madhara kwa mifugo ambayo ni moja ya nyenzo zao kuu kiuchumi, kwamba wanadhurika hata kufa.

Shida ni nini? Mwenyekiti wa Kitongoji cha Burongo kilichoko Kijiji cha Bisarwi, Juma Matinde, anaiambia Nipashe kuwa madhara hayo ya kiafya kwa binadamu na wanyama, pia mimea jirani, yamekuwa hali endelevu tangu kutokea anachokiita mkasa wa kuchafuliwa Mto Mara miaka minne iliyopita.

Kwa mujibu wa Matinde, hali hiyo imekuwa ikijitokeza tangu mwaka 2018 kila unapofika msimu wa mto kufurika, maji yake yamekuwa yakiwasha, wanapoyanywa tumbo linanguruma, wanaharisha, wanatapika na kukohoa, ikiendana na mikasa kadhaa ya kutapika na kuhara damu.

Nipashe imeambiwa kwamba, mifugo nayo ikitumia maji ya mto huo ambao ndiyo tegemeo pekee kwa wakazi na mifugo yao, imekuwa ikivimba tumbo, kulegea na hata kufa.

Mwenyekiti Matinde anasema pindi mifugo iliyodhurika ikichinjwa, waligundua nyama yake kuwa nyeusi na inayotoa harufu mbaya.

**WALIVYOIPOKEA**

Mwenyekiti Matinde anaeleza: "Hii ni wiki ya pili sasa kuna hali hii, tumesitisha kwa muda kula samaki, ng'ombe walipokufa siku za mwanzoni mwa mwezi huu, tuliwachinja na kuuziana nyama. Kila aliyekula alihara, yaani ukishakula, tumbo linanguruma kisha unaanza kuhara kidogo kidogo na kutapika.

"Zahanati iko mbali na hapa. Ukishagundua shida hii, unakwenda kwenye duka la dawa hapa kijijini, unawaeleza unavyojisikia, wanakupatia dawa."

Ushuhuda huo unajitokeza huku suala la uchafuzi wa Mto Mara mwanzoni mwa mwezi huu likichunguzwa na baadhi ya mamlaka za serikali kama vile Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria na kamati ya kitaifa iliyoundwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira.

**MKASA WA WAVUVI**

Mwenyekiti Matinde anasimulia kwamba wavuvi walipokuwa kazini mapema mwezi huu, walikuta samaki wakielea mtoni, wengi aina ya gogogo na sato.

Anasema baadhi yao waliothubutu kuwachukua ama kwa ajili ya kuuza ama kuwala, watumiaji wengi katika vijiji jirani waliharisha na kutapika.

Anasema muda mfupi baadaye, wavuvi hao waliufikishia taarifa uongozi wa maeneo yao kuwapo maji yenye mwonekano tofauti, meusi kwa rangi yakiashiria hatari kiafya na mazingira.

Hapo Mwenyekiti Matinde anasema viongozi walichukua hatua za tahadhari ikiwamo kuelimisha wananchi kwamba maji hayo na maudhui yake si salama kiafya, vinavyopatikana humo visiliwe.

Anasema wakati hatua hiyo inachukuliwa, baadhi ya watu walishakula vyakula vinavyopatikana kwenye maji hayo na kudhurika, ikiwamo nyama za mifugo iliyokufa kutokana na maji hayo.

"Viongozi tukapeleka taarifa ngazi ya juu serikalini, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Maji wakaja hapa na boti yao, wakaingia mtoni, wakachukua sampuli ya maji na samaki, wakapeleka maabara," Matinde anasema.

Mbali na kudokeza hata mbwa waliokula nyama za mifugo iliyokufa walidhurika, pia anasema binadamu walipokula samaki kutoka maji hayo, wana sifa hawachelewi kuharibika, pia wanakosa ladha iliyozoeleka kwa samaki na wana harufu mbaya.

Mwenyekiti anatoa takwimu alizonazo kwamba madhara kwa wanavijiji ni kudhurika kwa namna mbalimbali zilizotajwa, huku baadhi ya walioripoti wamewasilisha vifo vya ng'ombe 54 na mbuzi wanane katika kipindi cha wiki mbili za mwanzo wa mwezi huu.

Namna wanavyoshughulikia mifugo iliyokufa, Mwenyekiti Matinde anaeleza: "Kwa sasa mifugo inayokufa karibu na Mto Mara tunaitupa ndani ya maji, kwa inayokufa mbali na mto, tunachimba shimo na kuifukia."

**HATUA ZA KISERIKALI**

MWANZONI mwa mwezi huu kuliripotiwa kuwapo uchafuzi kwenye Mto Mara mkoani Mara uliosababisha samaki kufa na kuelea kwenye mto huo.

Iliripotiwa kwamba samaki walianza kuonekana Machi 8, mwaka huu, huku maji mtoni yakionekana kuwa na rangi nyeusi na juu kukiwa kumetanda kitu chenye mwonekano mithili ya mafuta, huku baadhi ya wakazi wakiokota samaki waliokufa na kuwauza kwa umma.

Vijiji vinavyotajwa kukumbwa na tatizo hilo ni pamoja na Kuruya, Kwibuse na Marasibora, baadhi ya wakazi wake wakikaririwa wakisema maji hayo yalikuwa yanatoa harufu ya uvundo yakiwa na utando wa kitu mithili ya mafuta.

Vijiji hivyo ni tofauti na ambavyo Nipashe ilipiga kambi siku chache zilizopita.

Baada ya uchunguzi wake kuhusu tukio hilo, Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria ilitoa matokeo ya utafiti ilioufanya kuhusiana na hali hiyo, ikibainisha samaki walikufa kutokana na kukosa hewa kulikochangiwa na kuwapo mafuta aina ya oili na grisi, yaliyotanda juu ya maji kwenye eneo la Kirumi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Rashid Tamutamu, pia alitangaza kuanza kwa uchunguzi wa kisayansi kupitia sampuli za samaki kujua undani wa mkasa wa vifo hivyo.

Vilevile, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Seleman Jafo, alitangaza kuunda kamati ya kitaifa kuchunguza suala hilo na Machi 19, mwaka huu, yalitangazwa matokeo ya utafiti kwamba, samaki hao walikufa kutokana na uchafuzi wa maji ya Mto Mara.

Katika ripoti yake hiyo, kamati hiyo ilitaja njia kuu mbili zilizochafua maji hayo, mosi ni kupitia mimea ya asili inayozalisha sumu, pia shughuli za kibinadamu zikijumuisha uwapo wa idadi kubwa ya mifugo iliyozalisha ziada ya kinyesi katika maji hayo.

**ITAENDELEA KESHO**

# MATANGAZO

## POSITION ANNOUNCEMENT
## FIELD OFFICER (Crop Productionist)
## IITA-TZ2022-R4D-004-NRS- MWANZA

**The International Institute of Tropical Agriculture (IITA)** is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit https://www.iita.org/ for more information on IITA.

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) has won a competitive two-year grant from **IFAD- South-South Cooperation (SSTC)** Facility to implement a project titled *'Supporting the Recovery of Priority Food Crop Value Chains from the Effects of COVID 19 to Strengthen Community Resilience, Markets, and Trade Development in Tanzania"*. The project will operate in the Central Corridor and part of the Lake Zone and will provide technical input and support to the IFAD-funded Agriculture and Fisheries Development Programme (AFDP). The two-year grant will be implemented in collaboration with the Alliance Bioversity International -CIAT (ABC) and other partners in target regions along the Central Corridor and part of the Lake Zone.

IITA-Tanzania office is seeking to recruit a qualified person to fill the vacancy of **the Field Officer (Crop Productionist)"** for the IITA-led IFAD-SSTC. The position requires a dedicated field officer to undertake field works that will ensure Quality seed producer network is strengthened and expanded to provide a delivery system for certified planting material, Good agronomic practices (GAP) promoted, and Efficiency of produce marketing maximized through facilitation of on-farm processing and marketing.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Mwanza, Tanzania.

**Overall Objectives**

The overall project goal is to restore and increase the productivity and profitability of key food and oilseed crops and enhance market access for rural women and young farmers in Tanzania to mitigate the negative impact of COVID-19 and enhance resilience. Specifically, the recruited Field Officer (Crop Productionist)" will implement field activities ensuring Boosting resilience of smallholder farmers through enhancing the productivity of cassava, sunflower, and beans in semi-arid and drought-prone areas.

**Scope of Work:**

The **Field Officer (Crop Productionist)"** will ensure the network of Quality seed producers is strengthened and expanded to provide a delivery system for certified planting material by identifying and promoting high yielding, disease-resistant, market suitable varieties. Train seed entrepreneurs, expand field certification to support new seed entrepreneurs, especially women and youth. Scale-out the application of the digital app to enhance seed certification and promote marketing of quality cassava seed. He will also Promote Good agronomic practices (GAP) including Digital technologies, train Farmers on-farm processing, and establishment of Marketing networks.

**Responsibilities:**

- Management and oversight of the production activities.
- Designing Implementing and monitoring of on-farm demonstration gardens
- Coordinating with the district staff to provide extensive knowledge to farmers
- Organize and conduct training for farmers and community extension staff
- Data collection, entry, analysis, and synthesis.
- Supervision and coordination of staff, students, and field labor
- Coordinate activities with project partners as may be necessary
- Coordinating with the nutrition and market teams to ensure cooperation
- Routine planning and reporting meetings
- Any other duties as may be assigned by supervisor
- Regular reporting

**Qualification and Experience**

- Bachelor's degree in agriculture or related field with 5 years working experience in Agricultural development.
- A strong ability to work within a team under minimum supervision and deliver results.
- Experience in data entry, data management, quality assurance, and timely reporting
- Proven knowledge of data collection tools including structured questionnaires.
- Ability to work in a multidisciplinary and multi-cultural environment
- Ability to liaise with other project implementing multi-disciplinary teams

**Skills Required:**

- Excellent communication skills in English and local language
- Computer proficiency including MS Office (Word/ PowerPoint, advanced excel skills, and SPSS)
- Ability to complete multiple tasks under pressure and meet deadlines

**General information:**

The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Mwanza. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

## POSITION ANNOUNCEMENT
## BUSINESS DEVELOPMENT AND MARKETING SPECIALIST - (Project Coordinator)
## IITA-TZ2022-R4D-003-NRS- MOROGORO

**The International Institute of Tropical Agriculture (IITA)** is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit https://**www.iita.org**/ for more information on IITA.

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) has won a competitive two-year grant from **IFAD- South-South Cooperation (SSTC)** Facility to implement a project titled ***'Supporting the Recovery of Priority Food Crop Value Chains from the Effects of COVID 19 to Strengthen Community Resilience, Markets, and Trade Development in Tanzania".*** The project will operate in the Central Corridor and part of the Lake Zone and will provide technical input and support to the IFAD-funded Agriculture and Fisheries Development Programme (AFDP). The two-year grant will be implemented in collaboration with the Alliance Bioversity International -CIAT (ABC) and other partners in target regions along the Central Corridor and part of the Lake Zone.

The second project titled BASICS II *(Building An Economically Sustainable Integrated Cassava Seed Systems)*, is funded by Bill and Melinda Gates Foundation with a vision of developing and commercializing the cassava seed supply chain—from the pre-basic seed of officially released varieties to the farmers through a network of government-certified commercial cassava seed entrepreneurs located throughout the primary cassava growing regions of Tanzania. It is a five-year project which has been operating in Nigeria since 2020 and now has been extended to Tanzania with effect from 2022.

IITA-Tanzania office is seeking to recruit a qualified person to fill the vacancy of the **Business Development and Marketing Specialist** (Project Coordinator) for the IITA-led IFAD-SSTC and BASIC-II projects' areas respectively.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Morogoro, Tanzania.

**Purpose and Overall Objectives**

The overall objective of the IFAD-SSTC funded project is to restore and increase the productivity and profitability of key food and oilseed crops and enhance market access for rural women and young farmers in Tanzania to mitigate the negative impact of COVID-19 and enhance resilience, and for BASICS II project is to provide farmers with access to affordable, quality-assured seeds of cassava varieties in demand by local food and processor markets through the establishment of a commercially viable seed value chain operating across breeder, foundation, and commercial seed levels. This value chain will enable more efficient dissemination and adoption of new varieties to improve productivity, raise incomes of cassava growers and seed entrepreneurs, enhance gender equity, and contribute to inclusive agricultural transformation in Nigeria and Tanzania."

**Scope of Work:**

Under IFAD -SSTC Project the Business Development and Marketing Specialist (Project Coordinator) will ensure the structured components are well coordinated by ensuring the boosted resilience of smallholder farmers through enhancing the productivity of cassava in drought-prone areas. Increased linkages between smallholder farmers and domestic and export markets in the cassava, beans, and sunflower value chains and manage the project, coordination of IITA-CIAT project activities, facilitate South-South collaboration, align the project activities with AFDP, gender integration, and M&E.

Subsequently, under the BASICS-II project, s/he will ensure Integration of Breeding and Seed System Activities, Development of Early Generation Seed Enterprises, Development of Commercial Seed Entrepreneurs, Development of the Processor-Associated Seed System Model, Quality Control and Disease Management and Catalysing Scaling and Replication through Partners. The coordinator will ensure the team's approach to achieving these outcomes is a continuation and strengthening of the innovative approaches undertaken during the current phases of BASICS-I and BEST but enhanced with changes informed by lessons learned over the past 5 years.

**Responsibilities:**

- Provide overall leadership and coordination of projects teams to ensure that project targets are achieved within the set timelines and corresponding budgets.
- Develop elaborate work plans for all actions and activities of the projects including preparation of planning, implementation, reporting, monitoring, and evaluation studies.
- For the IFAD-SSTC project, create efficient mechanisms for synergies and extensive sharing of knowledge between the project and the IFAD-funded Agriculture and Fisheries Development Programme (AFDP)
- Managing successful relationships with the government, donor agencies, the business community, related donor-funded projects, and other stakeholders as required
- Prepare the periodic financial and technical reports which include- quarterly, semi-annual, and annual reports.
- Establish and strengthen productive partnerships with the public (district) and private sector partners to facilitate learning and knowledge sharing.
- Organize coordination-planning and review meetings with the project implementing partners
- Work closely with the MEL officer to develop a performance management plan for the projects and monitor the implementation processes to track milestones.
- Ensuring daily management of the projects and assuming full accountability of projects results.
- Responsible for day-to-day operational coordination of partner activities,
- Contribute to the publication of action research results and success stories.
- Ensuring effective and efficient management of project's compliance with planning, monitoring, evaluation, performance, and reporting.
- Work closely with the projects Finance Administrator to ensure monitoring and strict budgetary adherence.
- Work closely with the projects Finance Administrator to review and ensure timely submission of regular financial reports
- Perform other activities as may be assigned by the supervisor.

**Qualification and Experience**

The candidate should have a master's degree relevant to general agriculture, agribusiness, and seed systems or its equivalent from a recognized university with experience in agricultural technology transfer, marketing, and management of partnerships.

A minimum of five years of senior level field experience in cassava productivity and seed business system

**Core Competencies:**

- Experience of at least 5 years as a project manager/ coordinator of large-scale agricultural development projects, in East Africa and Tanzania in particular.
- Having experience and a good understanding of production, markets, sustainable seed systems development, marketing challenges, and opportunities in Tanzania
- Demonstrated ability to integrate gender, youth, and private sector engagement issues into development projects
- Ability to work collegially and collaboratively in a multidisciplinary and multi-cultural environment.
- Demonstrated communication, networking, computer, and organizational skills and ability to prepare high-quality reports.
- Proven experience with engaging with public and private sector stakeholders
- Experience in marketing and business development skills is an added advantage
- Demonstrated ability in stakeholder and partner engagement and policy dialogue with an emphasis on district engagement.
- Excellent leadership, interpersonal and team-building skills.
- Excellent writing skills.
- Excellent resource mobilization skills

**General information:**

The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Morogoro. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe kukabili uchafuzi kwenye Mto Mara

**MWANZONI** mwa mwezi huu kuliripotiwa kuwapo uchafuzi kwenye Mto Mara mkoani Mara uliosababisha samaki kufa na kuelea kwenye mto huo.

Iliripotiwa kwamba samaki walianza kuonekana Machi 8, mwaka huu, huku maji ya mto huo yakionekana kuwa na rangi nyeusi na juu kukiwa kumetanda kilichodaiwa mafuta.

Vyombo vya habari nchini viliripoti kwamba baadhi ya wananchi walitumia fursa hiyo na kuingia mtoni na kuwaokota samaki kisha kuwauza kwa bei rahisi.

Vijiji vilivyodaiwa kukumbwa na tatizo hilo ni pamoja na Kuruya, Kwibuse na Marasibora, baadhi ya wakazi wake wakikaririwa wakisema maji hayo yalikuwa yanatoa harufu yenye ishara za kitu kilichooza na yalikuwa na utando wa kitu kama mafuta.

Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria ilitoa matokeo ya utafiti wa sampuli za maji waliyopima katika maabara yao kuhusiana na uchafuzi huo, ikibainisha samaki hao walikufa kutokana na kukosa hewa ya oksijeni kutokana na kuwapo mafuta aina ya oili na grisi yaliyotanda juu ya maji eneo la Kirumi.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo maofisa wake walizuru kwenye maeneo yaliyochafuliwa, ilitangaza kuanza kwa uchunguzi kwa kuchukua sampuli za samaki hao na kuzipeleka kwenye maabara ya usalama wa chakula mjini Musoma ili kujua chanzo cha vifo hivyo.

Vilevile, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ambayo pia maofisa wake wa juu walizuru eneo la tukio, ilitangaza kuunda kamati ya kitaifa kuchunguza suala hilo.

Machi 19, mwaka huu, kamati hiyo ya kitaifa ilitangaza matokeo ya utafiti wake, ikibainisha kuwa samaki hao walikufa kutokana na uchafuzi wa maji ya Mto Mara.

Katika ripoti yake hiyo, kamati hiyo ilibainisha njia kuu mbili za uchafuzi za asili kama vile mimea kuoza na hivyo kuzalisha sumu pamoja na shughuli za kibinadamu zikijumuisha uwapo wa idadi kubwa ya mifugo iliyozalisha tani milioni 1.8 za kinyesi.

Nipashe kama mdau wa afya na mazingira, tumefuatilia kilichoripotiwa na mamlaka mbalimbali za serikali kuhusu uchafuzi huo, pia tukitembelea maeneo yaliyoripotiwa kuathirika zaidi na kuzungumza na wakazi wake. Kwenye maeneo hayo ya waathirika wa uchafuzi huo, tulibaini kuwapo taarifa za vifo vya mifugo (ng'ombe na mbuzi) ya wakazi wa maeneo hayo vinavyodhaniwa kutokana na kunywa maji ya Bonde la Mto Mara yanayopita karibu na maeneo yao.

Baadhi ya wakazi wa maeneo hayo walidai kwamba walipokula samaki waliokufa kutokana na uchafuzi huo, walipata madhara kiafya, ikiwamo kuhara na kutapika.

Tukizingatia ripoti zote zilizotolewa na mamlaka za serikali kuhusu suala hilo zinabainisha kuwapo uchafuzi kwenye Mto Mara, Nipashe tunaona kuna haja serikali kuchukua hatua kukabiliana na madhara ya uchafuzi huo kwa binadamu, mifugo na mazingira.

Nipashe tunaamini kuna haja kupata mwarobaini wa kuzuia shughuli za kibinadamu zinazosababisha uchafuzi kwenye Mto Mara, ikizingatiwa kwamba kumekuwa na matukio mengi yanayohusisha uchafuzi ndani ya mto huo.

Shime, uchafuzi kwenye Mto Mara unapaswa kudhibitiwa kwa kuwa mbali na kutumiwa kama chanzo kikuu cha maji na sehemu ya kujipatia kitoweo cha samaki kwa wakazi wa maeneo unakopita, mto huo unaingia Ziwa Victoria ambalo maji yake yanatumiwa na mamilioni ya wakazi wa Kanda ya Ziwa.

Tunaona kwamba kuna sababu kwa kila mdau kujikita katika ufumbuzi wa tatizo hili badala ya kulitumia kujinufaisha kibinafsi kisiasa au kwa njia zingine za kupata fursa. Tunasema hivyo kutokana na namna makundi kadhaa ya kijamii yanavyokinzana kwa kutoa kauli zinazoonekana kutokuwa na uhalisia wake. Kwa kuwa linahusu afya za binadamu na viumbe wengine, ni vyema yakatangulizwa mbele maslahi ya taifa badala ya binafsi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili la daladala Mwanza kukatiza 'ruti' linakera kuliko maelezo

Na Anthony Gervas, Mwanza

**BAADHI** ya madereva, kondakta wa daladala za mabasi madogo jijini Mwanza, mnaofanya safari njia ndefu kwanini mmegeuka kero kubwa kwa abiria, mnakatisha 'ruti' za safari kabla ya gari kuwafikisha kwenye kituo husika.

Nauliza hivi hamuoni kwamba mnawasababishia wateja wenu usumbufu na kero ya kulipa nauli mara mbili kinyume cha sheria, kwanini mnageuzia magari njiani na kuwashusha abiria kibabe, huku mkiwatolea lugha chafu na vitisho, kuwadhalilisha wakati leseni zenu zinawataka mfanye safari hadi kituo cha mwisho.

Tabia hii mmeitoa wapi? Iwe asubuhi, mchana na jioni sasa ndiyo usiseme, mnatoa hadi vitisho vya kutaka kuwapiga abiria bila kujali utu wanapodai haki zao za kufikishwa kwenye vituo husika, nafikiri kuna haja ya kunyang'anya leseni hizo sababu mnaonekana mmechoka kutoa huduma hiyo.

Katika jiji hili magari ya njia ndefu ni pamoja na yanayofanya safari zake kutoka uwanja wa ndege kwenda Kisesa, Nyashishi hadi Kishiri, kutoka Kisesa kwenda Nyashishi - Usagara, pia Nyashishi kwenda Uwanja wa Ndege. Hawa ndiyo vinara wa kukatisha safari za abiria.

Mimi nasema hakuna mteja aliyekwenda kwa wahusika Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuwaombea leseni ya kusafirisha, mlikwenda wenyewe mkapewa mkaridhika kwenda safari za njia ndefu, halafu tena mnaanza kutusumbua kwa visingizio mara eti gari ni bovu haliwezi kufika kituo cha mwisho wakati liko barabarani.

Kama unajua gari lako bovu, kwanini umelileta barabarani kutoa huduma hiyo, badala ya kulipeleka gereji kutengenezwa, unataka kutupotezea maisha yetu bila ya sababu za lazima, wala hamwogopi mkono wa sheria za usalama barabarani nani kawaroga?

Kazi yangu wiki hii mimi binafsi ni kukemea upuuzi huo unaofanyika katika jiji letu la Mwanza, utasikia kondakta na dereva wake wakitangaza eti "gari haliendi hadi huko tunaishia Igoma hatufiki Kisesa' mara tena 'tunaishia Pasiansi au Buhongwa hatufiki Nyashishi'.

Wanatoa tangazo hilo bila kuogopa sheria, wateja wakiuliza wanaambiwa gari hilo ni bovu, linatakiwa kupelekwa gereji au kwa fundi wakati limepakia abiria na linaendelea kupakia wale wanaoishia lilipotangaza kugeuzia.

Lakini, ukiandika namba zake na kulifuatilia kama kweli limepelekwa kutengenezwa, utaona linapita tena barabarani likiwa limepakia abiria hadi wamesimama mpaka mlangoni mwa kondakta likirudi lilikotoka. Lini tabia hiyo itakomeshwa na mamlaka husika sababu ni kero kwetu wateja.

Ndiyo maana nauliza tabia hii ya uongo na uvunjifu wa sheria za usalama barabarani kwa hawa wenye magari wanazitoa wapi? Kwenye majiji makubwa kama letu, hawajifunzi kutoka katika majiji mengine kama vile Dar es Salaam. Dereva na kondakta hawawezi kufanya ulaghai kizembe kwa abiria bila ya sababu za msingi.

Naomba abiria tuwe na ushirikiano wa pamoja, kuhakikisha hatunyanyaswi na madereva au makondakta tunapopanda magari hayo, sababu tunalipa nauli halali ili tupate huduma ya usafiri ambayo ni haki yetu. Tukatae kushushwa njiani kabla hatujafika vituo vyetu tunavyokwenda.

Pia kama haitoshi wahusika watoe namba za simu kwenye kila gari la daladala hizo, ili abiria iwe rahisi kutoa taarifa kituo cha polisi au kwa askari wa usalama barabarani, aweze kupata msaada zaidi au LATRA.

Wananchi wanatupia lawama zao kwa baadhi ya askari wa usalama barabarani kuwa hawasimamii vema sheria, sababu na wao ni sehemu ya umiliki wa magari ya daladala, namdokeza mkuu wa kitengo cha usalama barabarani mkoani hapa afuatilie na kutatua kero.

Kwa leo dozi yangu imetosha tukutane tena siku nyingine bila kumung'unya maneno, zama hizi za ukweli na uwazi, kurunzi langu linaishia hapo kuwamulika wahusika kila mmoja kwa nafasi yake.

TANGAZO

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

# Majaribu Yaliyokumba Vyama; Matumaini, Sheria na Zama Mpya

**Mwandishi wetu, LHRC**

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kukusanyika kwa ajili ya jambo fulani kwa jamii ni haki ya msingi, ambayo kila raia wa Tanzania anastahili kuipata bila kuzuiwa.

Katiba, katika ibara ya 20(1) inasema, "Kila mtu anastahili kuwa huru, bila ya kuathiri sheria za nchi, kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika na kushirikiana na watu wengine, kutoa mawazo hadharani, na hasa zaidi kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo."

Tanzania imeridhia mikataba ya kimataifa ukiwemo wa kimataifa haki za kiraia na kisiasa (ICCPR) na mkataba wa Afrika wa Haki za binadamu (ACHPR)

Licha ya haki hiyo, bado kumekuwa na vikwazo vingi vinavyosababishwa na sheria na matamko ya viongozi wa Serikali.

Uhuru wa kukusanyika ulipata pigo zaidi katika Awamu ya Tano ya Hayati Rais John Magufuli aliyepiga marufuku mikutano ya vyama vya siasa na maandamano.

Kama hiyo haitoshi, Sheria ya Vyama vya Siasa ilifanyiwa marekebishi mwaka 2019 na kuongeza ugumu zaidi wa vyama kukusanyika.

**Asasi za kiraia**
Ripoti ya Haki ya Watetezi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa siasa nchini iliyotolewa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) inagusia Mabadiliko ya Sheria mbalimbali ya mwaka 2019 ambayo pamoja na mambo mengine yalirekebisha Sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) ya mwaka 2002 na Sheria ya vyama vya kiraia na kampuni yam waka 2002.

"Sheria hizo tatu ndiyo zilikuwa muhimu katika kusajili na kudhibiti Asasi za Kiraia Tanzania (CSO) na baada ya marekebisho hayo, hakuna NGO iliyoruhusiwa kusajiliwa kama kampuni" imeeleza Ripoti ya Haki ya Watetezi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa siasa nchini iliyotolewa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC)

Awali sheria hizo zilipokelewa vizuri kwani CSOs sasa zinaweza kusajiliwa kama NGOs na itakuwa rahisi kuziratibu. Hata hivyo, CSOs zilipewa muda wa siku 30 kusajiliwa, jambo lililokuwa gumu na kusababisha nyingi kufa.

**Haki za kisiasa**
Katiba ya Jamhuri ya Muungano ibara ya 21(1) ikiwa pamoja na vifungu vya 39, 47 na 67 vinavyotoa haki ya kila mwananchi kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi au kuteua na kuteuliwa katika masuala ya uongozi iwe moja kwa moja au kwa kuwakilishwa.

Kifungu kidogo cha (2) cha ibara hiyo kinasema, kila raia ana haki na uhuru wa kushiriki mchakato wa kufanya uamuzi kwa mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au Taifa.

Sheria ya Vyama vya Siasa iliyorekebishwa mwaka 2019 nayo imetoa haki kwa viongozi wa vyama vya siasa kushiriki kwenye shughuli za siasa kwa mujibu wa sheria.

"Pamoja na Katiba na sheria nyinginezo kutoa haki hizo, kumekuwa na zuio la kufanyika kwa shughuli za siasa nchini tangu mwaka 2019. "Viongozi wa vyama vya upinzani wamelengwa katika zuio hilo. Wamekuwa wakizuiwa kutfanya shughuli za kisiasa ikiwemo mikutano ya ndani na nje, kwa kisingizio cha kulinda Amani," imesema sehemu ya ripoti hiyo.

Sheria ya Jeshi la Polisi na Jeshi la huduma ndogo (Police Force and Auxiliary Services Act 2002) ndiyo imekuwa ikitumika kukandamiza hhaki ya vyama na makundi mengine kukusanyika, kwani inataka wanaotaka kukusanyika kutoa kwanza taarifa kwa Jeshi la Polisi angalau saa 48 kabla ya mkusanyiko huko.

Jeshi hilo limekuwa likitumia mamlaka hiyo katika matukio tofauti ikiwa pamoja na kuzuia mikutano ya vyama vya siasa na makundi mengine zikiwemo asasi za kiraia.

Hata hivyo, ripoti hiyo inasema zuio hilo ambalo pia liko kinyume na sheria, linaonekana kutofanya kazi kwa chama tawala CCM, kwani kimekuwa kikifanya mikutrano sehemu mbalimbali na kikipewa ulinzi na Polisi.

"Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya siasa ya mwaka 2019 yamekuwa pia kikwazo, kwani yameweka zuio kwa majukumu ya msingi ya vyama vya siasa na watendaji wengine wa vyama bila kufuata utaratibu uliomo ndani ya sheria hiyo.

"Madaraka ya Msajili wa Vyama vya Siasa yameongezwa, kiasi kwamba sasa anasimamia utoaji wa elimu ya uraia, kufuta vyama na kuingilia mambo ya ndani ya vyama. Kimsingi madaraka hayo yanazorotesha mchakato wa demokrasia."

Ripoti ya Haki za Binadamu ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ya mwaka 2018 imetaja baadhi ya matukio yanayokwamisha haki ya kukusanyika likiwemo la kukamatwa na kushitakiwa kwa viongozi wa Chadema kwa madai ya uchochezi.

Viongozi wa Chadema waliokamatwa mwaka 2018 ni pamoja na Mwenyekiti Freeman Mbowe, Vincent Mashinji (sasa amehamia CCM), John Mnyika, Peter Msigwa, Esther Matiko, Salum Mwalimu, and Halima Mdee.

Viongozi hao walikamatwa kufuatia maandamano waliyoyaongoza baada ya mkutano wa kampeni ya uchaguzi wa marudio katika jimbo la Kinondoni Februari 16, 2018, ambapo walikuwa wakidai fomu kwa ajili ya mawakala wa chama hicho zilizotakiwa kutolewa na Mkurugenzi wa manispaa ya Ilala.

Kesi hiyo imeamuliwa Machi 10, 2019 ambapo viongozi hao walihukumiwa kwenda jela au kulipa zaidi ya Sh350 milioni. Hata hivyo, fedha hizo zilichangwa na wanachama na wakatolewa jela.

Mbali na vyama vya siasa, ripoti ya LHRC imebainisha kuwepo kwa vitisho kwa wananchi waliotaka kuandamana.

"Aprili 2018 wananchi walitishwa na Jeshi la Polisi kuwa watapata kipigo cha 'mbwa koko' na watapata taabu sana kama wangeshiriki kwenye maandamano yaliyopangwa kufanyika Aprili 26, 2018 ambayo ilikuwa ni siku ya sherehe za Muungano.

"Vitisho hivyo ndiyo vimechangia kujenga hofu kwa watu kushiriki kwenye maandamano. Utafiti uliofanywa na Twaweza umeonyesha kuwa watu wawili kati ya watu waliohojiwa walisema hawatashiriki kwenye maandamano hayo," imesema ripoti hiyo.

Vyama vya siasa hasa vya upinzani vimekuwa vikilalamikia Jeshi la Polisi kuingilia mikutano yao ya ndani na ya nje.

Miongoni mwa mikutano iliyozuiwa na Jeshi la Polisi ni mkutano wa ndani wa Chadema wilayani Sengerema mkoani Geita Machi 5, 2020, sababu ikitajwa kuwa ni taarifa za kiinteljensia kwamba katika mikusanyiko hiyo kuna vitisho.

Januari 14, 2020, Jeshi la Polisi lilizuia mkutano wa habara uliopangwa kufanywa na kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini kwa madai ya taarifa hizo za kiinteljensia za usalama.

Polisi pia wameshazuia mikutamo ya hadhara ya wabunge wa vyama vya upinzani wakiwemo Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi kwa madai ya taarifa za kiusalama.

Hata hivyo, wakati jeshi hilo likizuia mikutano hiyo, halijawahi kuwabugudhi viongozi wa CCM wanapofanya mikutano yao iwe ni ya ndani au ya hadhara.

**Zama mpya**
Baada ya Rais Samia Suluhu kuingia madarakani Machi 2020, kumekuwa na ahueni kwa makundi ya siasa na vyama vya kiraia vilivyokuwa vikidai kunyiwa uhuku wa kukusanyika na kufanya kazi zao.

Mkutano wa vyama vya siasa ulioandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kufanyika jijini Dodoma Desemba 15-17, 2021 umeonyesha dhamira ya maridhiano ya kisiasa na kiraia.

Hata hivyo, mkutano huo uliohutubiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ulisusiwa na vyama vya Chadema na NCCR Mageuzi vikidai kukutana na Rais mwenyewe kufanya mazungumzo.

Kwa upande mwingine, ACT Wazalendo pamoja na vyama vingine vilivyoshiriki vimeweka msimamo wa kudai Tume huru ya uchaguzi kabla ya kupatikana kwa Katiba mpya.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Juma Duni Haji alisema ataongoza mapambano ya kupigania Tume huru ya uchaguzi na katiba mpya kwa sababu limekuwa ni hitaji la wananchi tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi.

"Tunaamini kuwa kwanza tunapaswa kuwa na Tume huru ya uchaguzi itakayosimamia kura ya maoni ya katiba mpya na itakayohakikisha kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 unakuwa huru, wa haki na wa kuaminika," alisema.

# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

## Sheria Kandamizi Zilivyo Mwiba kwa Uhuru wa Kujieleza

**Mwandishi wetu, LHRC**

Licha ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR) la mwaka 1948 katika ibara ya 19 kutambua uhuru wa kujieleza kama haki ya kila mtu, uhuru huo unaminywa sehemu nyingi duniani.

Uhuru huu unahusisha kuwa na maoni bila kuingiliwa na kutafuta, kupokea na kuwasiliana au kuwasilisha taarifa na mawazo yake kupitia vyombo vya habari bila kujali mipaka, iwe ni kwa kuongea au kwa kuandika au kuchapisha kwa njia ya sanaa au kwa njia yoyote ya vyombo vya habari.

Pia, huu umeainishwa katika Tamko la kimataifa la haki za kiraia na kisiasa (ICCPR) la mwaka 1966 na Mkataba wa Afrika wa Haki za watu na Binadamu ambao katika ibara ya 9 (1&2) unasema kila mtu ana haki ya kupokea taarifa na kila mtu anayo haki ya kujieleza na kutoa maoni yake ndani ya sheria.

Kwa Tanzania, kama zilivyo sehemu nyingine, uhuru huo hata hivyo umekuwa ukiminywa na Serikali na pande nyingine katika nyanja na vipindi tofauti.

Tanzania imeridhia mikataba ya ICCPR na ACHPR kwa hiyo inajifunga na masharti ya mikataba hiyo hivyo hata sheria zake zinapaswa kufuata miongozo hiyo.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano ibara ya 18(1) inasema: "Bila ya kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, na kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi, na pia ana uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati."

"(2) Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii."

Licha ya haki ya kujieleza kutambuliwa na Tanzania, bado kumekuwa na changamoto za upatikanaji wa haki hiyo.
Kwa mujibu wa RSF, Tanzania imekuwa ikianguka tangu mwaka 2016 ambao ilikuwa nafasi 71 kati ya nchi 180. Mwaka 2017 ilishuka hadi nafasu ya 83, mwaka 2018 ilishika nafasi ya 93, mwaka 2019 nafasi ya 118 na 2021 Tanzania imeshika nafasi ya 124.

Hata hivyo, taarifa iliyotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) Desemba 31, 2021, Dar es Salaam imeonyesha kupungua kwa matukio ya waandishi wa habari kukamatwa na vyombo vyao kufungiwa na kupigwa faini matukio Katika kipindi cha mwaka 2021, ukilinganisha na mwaka 2020.

"Katika kipindi cha mwaka 2020 jumla ya waandishi 13 walikamatwa, vyombo kumi vya habari vilipigwa faini wakati vyombo vya habari vinne vilifungiwa. Hali hiyo ni tofauti na mwaka 2021 ambapo waandishi wa habari waliokamatwa walikuwa saba, na vyombo vya habari viwili vilifungiwa," imesema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo imeelezea kuwa madhila ambayo MCT inayarekodi ni yale ambayo yaliripotiwa kwa njia ya simu au kuchapishwa kwenye vyombo vya habari au mitandao ya kijamii au kuripotiwa kwa washirika wake.

"Matukio ya ukiukwaji wa haki za waandishi wa habari (madhila) ambayo Baraza linarekodi ni kunyimwa taarifa na chanzo cha habari, vitisho, mauaji ya waandishi wa habari yanayohusishwa na kazi zao, kufungiwa kwa chombo cha habari na kupigwa faini", taarifa ya MCT imeeleza.

Imeongeza kuwa: "Mengine ni shambulio kwa mwandishi wa habari akiwa kazini, vifaa vya mwandishi wa habari kuharibiwa akiwa anatimiza majukumu yake, kuondolewa katika eneo la tukio akiwa anatimiza majukumu yake kusikofuata sheria na taratibu zilizopo…'

Aidha, taarifa hiyo imesema kuwa kumekuwa na kuingiliwa kwa uhuru wa uhariri na hali ya vyombo vya habari kuogopa kutumia habari fulani kwa hofu ya mamlaka au watoa taarifa.

Kwa mujibu wa Kanzi data ya MCT, katika kipindi cha mwaka 2020 ilirekodi matukio ya ukiukwaji wa haki za waandishi wa habari 43 wakati mwaka 2021, imerekodi matukio 25 mpaka Disemba 27, 2021.

Taarifa hiyo imeungwa mkono na maoni ya Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile akisema hali ya uhuru wa vyombo vya habari imeanza kuimarika.

"Hali ya uhuru wa vyombo vya habari imeanza kuboreka. Bado mambo machache ikiwemo kufungulia magazeti yaliyofungiwa. Hilo ndilo limebaki kuwa gumu," alisema.

Hata hivyo, Balile alisema Serikali (Wizara ya Mawasiliano Teknolojia na Habari) ilishakutana na wamiliki wa magazeti hayo na kuafikiana mambo kadhaa wakati huo Waziri akiwa Dk Ashatu Kijaji.

"Hata Waziri wa sasa Nape Nnauye ameshasema vizuri sana, kwamba anajua shida iliyopo katika vyombo vya habari wala waandishi wa habari na alikwenda mbali zaidi akisema hatamwangusha Mungu na jumuiya ya kimataifa na matumaini ya Rais Samia (Suluhu Hassan) aliyesema vyombo vya habari vifunguliwe," alisema Balile.

Aliendelea kusema; "Kwa ujumla ukiangalia kuna mabadiliko makubwa sana. Yapo masalia askari mmoja au wawili, lakini kwa ujumla ukiangalia kati ya Machi 2021 na sasa Januari 2022, kuna mabadiliko mazuri sana."

**Sheria kandamizi**
Licha ya matukio hayo kupungua, uhuru wa kujieleza pia ilipata pigo baada ya kupitishwa kwa sheria kandamizi zikiwemo za Sheria ya Huduma za Habari ya 2016, Sheria ya Takwimu (2016), Sheria ya Makosa ya Mitandao (2015).

Mwaka 2018 LHRC ikishirikiana na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na THRDC walifungua kesi mahakama Kuu Kanda ya Mtwara wakipinga kanuni za maudhui ya mtandao (Epoca) wakipinga madaraka makubwa aliyopewa Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo kuwa na nguvu kubwa katika kanuni hizo.

Hata hivyo Mahakama kuu Kanda ya Mtwara ilitupilia mbali zuio la kutumia kanuni hizo na kuipa Serikali ushindi.

Hata hivyo, kabla ya hapo mashirika hayo yalikuwa yamefungua kesi nyingine katika Mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ) yakipinga baadhi ya vipengele vya Sheria ya Huduma za Habari.
Hatimaye Machi 2019 EACJ iliyapa ushindi mashirika hayo ikisema sheria hiyo inakiuka uhuru wa kujieleza pia inapingana na Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambao Tanzania imeuridhia.

Kesi hiyo namba 2 ya mwaka 2017 ilifunguliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kituo cha Msaada wa Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) wakilalamikia ukandamizaji wa uhuru wa habari.

Vipengele vilivyolalamikiwa vipo 18, ambavyo ni pamoja na (3)(a), 13, 1920, 21,34, ambapo pamoja na vifungu vingine, walalamikaji walisema vinakiuka utawala bora, demokrasia na utawala unaozingatia sheria na inapingana na mkataba ulioanzisha EAC.

Hata hivyo, bado Serikali haijarekebisha vipengele vya sheria hiyo licha ya kushindwa kesi mahakamani.

## Katibu mkuu wizara madini aridhishwa GGML uzingatiaji wa sheria

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Madini, Adolph Ndunguru, ameipongeza kampuni ya GGML kwa kuzingatia sheria zinazosimamia sekta ya madini na kutekeleza majukumu yake kwa uweledi.

Ndunguru alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na menejimenti ya GGML baada ya kufanya ziara katika kampuni hiyo kwa mara ya kwanza.

"Tangu Rais Samia Suluhu Hassan aliponiteua kwenye wadhifa huu, nimesikia maoni mengi mazuri kuhusu GGML.

Nakumbuka hivi karibuni mlipokea zawadi na tuzo nyingi kule mkoani Dar es Salaam. Tuzo hizo zilikuwa zinatambua utendaji kazi wenu kama kampuni bora ya uchimbaji madini kwa mwaka 2021.

Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti anayesimamia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo, alimshukuru Ndunguru kwa kutembelea mgodi huo.

Alieleza kuwa GGML itaendelea kuzalisha katika mazingira uendelevu kwa kulipa kodi na kuchangia programu mbalimbali za uwekezaji ndani ya jamii zinazosaidia wananchi wanaozunguka mgodi.

"Tumekuwa na changamoto nyingi katika shughuli zetu ikiwa ni pamoja na kupungua kwa madini yanayochimbwa kupitia uchimbaji wa wazi katika mgodi wa Nyankanga.

"Pia kulikuwa na ucheleweshaji wa utoaji wa vibali vya uchimbaji wa wazi Mlima wa Geita na Nyamulilima.

Tunashukuru kwamba sasa tuko katika hatua nzuri kwani uendelezaji wa miradi yote miwili ulianza mwaka 2021," alisema.

# Ridhiwani amshukuru Samia kutatua kero ya maji Chalinze

**Frank Monyo na Julieth Mkireri,** PWANI

MBUNGE wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumaliza kero ya maji katika jimbo hilo iliyokuwa ikiwatesa wananchi kwa zaidi ya miaka 50.

Ridhiwani, alitoa shukrani hizo juzi mbele ya Rais Samia wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Maji Mlandizi - Chalinze - Mboga uliotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa gharama ya shilingi bilioni 18.

"Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Rais, leo hii nasimama kwa furaha kubwa sana nikiona maneno niliyoyasema wakati wa kampeni leo hii yanaenda kutekelezwa, mradi wa maji Chalinze umekamilika lakini nikushukuru sana wewe kwa kuhakikisha mradi hii unakamilika kwa kiwango kikubwa," alisema Ridhiwan na kuongeza:

"Wanasema usipomshukuru binadamu mwenzako huwezi kumshukuru Mungu usiyemwona, kwa nafasi hii ya kipekee naomba nimshukuru Hayati Dk. John Pombe Magufuli kwa kuanzisha mradi huu maana mradi huu ni mafanikio ya utekelezaji wa ilani ya chama chetu."

Rais Samia akihutubia wananchi waliojitokeza katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Maji baada ya kuzindua mradi huo aliahidi kutoa shilingi milioni 500 kwa DAWASA kwa ajili ya kusambaza huduma ya maji kwa wananchi wa eneo hilo baada ya kukamilika kwa mradi huo utakao hudumia wakazi zaidi ya 120,000.

Alisema: "Tunataka maji haya yawafikie wananchi, tunaanza na milioni 500 zitakuja DAWASA kuanza kazi ya usambazaji wa huduma ya maji kwa wananchi, tunaanza na hizo tukiangalia kasi yenu, kama kasi ikiwa nzuri tutaongeza nyingine milioni 500," alisema Rais Samia na kuongeza:

"Lakini fedha hii DAWASA mnakuja kuirudisha kwa sababu wananchi watawalipa bili, mtarudisha kwenye mfuko niliyotoa, eeh kwa hiyo hii ni mkopo, nitatoa milioni 500 na baadaye nitaongeza milioni 500 ili kazi ya usambazaji maji kwa wananchi iweze kufanyika. "Maji haya sio sadaka DAWASA inafanya biashara hivyo niwaombe mlipe bili za maji. Bili hizi zitakuwa na unafuu mkubwa kuliko mnavyolipa maji sasa hivyo lipeni bili ili Dawasa iweze kuwadumia," alisema Samia.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutamaliza changamoto ya upatikanaji wa maji kwani unauwezo wa kuzalisha lita milioni 9.3 kwa siku na kuhudumia zaidi ya wakazi 120,000 na kufanya hali ya upatikanaji wa maji Chalinze kufikia asilimia 76.

Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Julai 2019 na kukamilika kwa mradi huo unakwenda kumaliza kero ya maji iliyokuwapo Chalinze kwa muda mrefu.

Mhandisi Luhemeja alisema katika mradi huo lita milioni 9.3 zitakuwa zinasambazwa kwa wananchi zaidi ya 120,912 kwa siku.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema pamoja na serikali kuweka fedha nyingi kwenye mradi wa Maji Chalinze, lakini miradi imekuwa ikisuasua.

"Kulikuwa na Mamlaka ya Maji inasimamia Chalinze inaitwa CHALIWASA, ilikuwa inaomba fedha kwa ajili ya dawa (kisafishia maji) miundombinu lakini wananchi walikuwa hawana huduma ya maji, Mh Rais sikusita kuifuta mamlaka hiyo kwa maslai mapana," alisema Aweso.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alimshukuru Rais Samia kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kumaliza kero za wananchi ikiwamo sekta ya maji.




Dk. Joseph Chacha Sunguro (kushoto) wa Hospitali ya CCBRT, akimpima macho mmoja wa wakazi wa Kunduchi, Dar es Salaam, katika zoezi la uchunguzi wa afya ya macho na magonjwa ya mifupa, lilioendeshwa kwa pamoja kati ya hospitali hiyo na kituo cha afya cha Jeshi la Polisi Kunduchi jana, ambapo zaidi ya wakazi 100 wa eneo hilo, walipatiwa huduma hiyo. Tangu mwaka 2020 taasisi hizi mbili zimekuwa zikishirikiana katika kutoa huduma za afya kwa Watanzania wenye mahitaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walalamikia kuchangia maji na mifugo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya wakazi wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga wanalazimika kutumia maji ya visima vya kienyeji wakichangia na mifugo kutokana na ukosefu wa huduma ya majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria.

Malalamiko hayo yalitolewa wakati wa ziara yake ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, kukagua miradi ya maji inayotekelezwa katika Halmashauri ya Msalala na Ushetu kwa thamani ya zaidi ya Sh. bilioni nne.

Mkazi wa Kata ya Mwanase, Maisha Raphael, alisema kutokana na tatizo la kukosa huduma hiyo wanalazimika kutumia maji yasiyokuwa salama.

Alisema wakati mwingine wamekuwa wakiamka alfajiri kuelekea kata za jirani kuchota maji na kurejea majumbani saa tatu asubuhi na kuiomba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuwahimiza makandarasi kukamilisha miradi kwa wakati ili kuwaondoa shida hiyo.

Naye Maliam Simon alisema watembea kilometa 15 kwenda na kurudi kutoka Kata ya Mwanase hadi Kashishi kwenda kuchota maji na wasiokuwa na uwezo wa kufika wakiwamo wajawazito wananunua maji lita 20 kwa Sh. 1,000.

Kaimu Meneja wa RUWASA, Paschal Mnyeti, akitoa taarifa ya ujenzi wa miradi ya maji alisema kuna miradi ya maji inayoendelea kujengwa katika Halmashauri za Msalala na Ushetu ya zaidi ya Sh. bilioni nne ambayo itamaliza tatizo la kukosekana kwa huduma ya maji.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo unachukua kipindi kirefu kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha pamoja na kukosa njia za kupitisha vifaa vya ujenzi husussani kipindi cha mvua za masika.

Mnyeti aliwataka makandarasi wanaoendelea kujenga miradi ya maji kuhakikisha wanajenga vituo nane vya kuchotea maji pamoja na mabilika mawili kwa ajili ya kunyweshea mifugo na atahakikisha ujenzi wake unakamilka kwa wakati uliopangwa.

Kwa upande wake, Kiswaga alisema hadi kufikia April 30, mwaka huu, makandarasi wote wahakikishe miradi yote ya maji inayoendelea kujengwa iwe imekamilika na atayeshindwa atawajibishwa kisheria kwa kukatwa fedha na kunyang'anywa mradi.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya kusambaza mtandao wa majisafi na salama kwa wananchi hususani wale wanaoishi pembezoni mwa miji.

# Shirika lataka hadhari ya kirusi kipya corona

**Na Sabato Kasika**

JAMII imeshauriwa kuchukua tahadhari zote zinazoelekezwa na Wizara ya Afya ili kujikinga na UVIKO-19, kutokana na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuthibitisha kuwapo kirusi kipya cha ugonjwa huo.

Ushauri huo umetolewa na Mwenyekiti wa Shirika lisilo la Kiserikali la Eden Twins Foundation ambalo linalotoa huduma za kijamii kwa wazazi wenye watoto mapacha, lakini hawana uwezo kiuchumi, Diana Mbena.

Akizungumza na gazeti hili mkoani Dar es Salaam jana, alitaja tahadhari hizo kuwa ni pamoja na wananchi kujitokeza kuchanjwa na pia kuzingatia maelekezo ya mwongozo wa wizara hiyo ya jinsi ya kujikinga na UVIKO-19.

"Nimemsikia Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akizungumza na waandishi wa habari na kuthibitisha kuwa kirusi kipya hakijaingia nchini. Hiyo taarifa njema kwa Watanzania, lakini amegusia suala la kuchukua tahadhari," alisema Diana.

Mwenyekiti huyo alisema, suala la tahadhari ni la muhimu, na kufafanua kuwa kwa vile kirusi hicho kimeshaingia kwenye baadhi ya nchi, inawezekana kikaingia Tanzania iwapo wananchi hawatachukua tahadhari.

"Tuendelee kukumbushana, nasi Eden Twins Foundation tunashauri tahadhari zichukuliwe kwa kuchanja, kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kunawa maji tiririka, kuvaa barakoa na kutumia vitakasa mikono," alisema.

Alisema, anahimiza hilo kutokana na kwamba, baadhi ya watu wamekuwa hawatilii maanani kuwapo kwa UVIKO-19 nchini, hali ambayo inayoweza kusababisha wakakumbwa na ugonjwa huo.

Alisema kwa kuwa shirika lake linahudumia watu ambao wengi wao hawana uwezo kiuchumi, ni vyema wapate huduma ya chanjo ili kuwa salama, kwa kuzingatia kwamba inatolewa bure.


"Maelezo ya Waziri Ummy ni kwamba serikali inataka kuhakikisha wananchi wanapata chanjo ya UVIKO-19, kwa kuwa ni vigumu kukwepa ugonjwa huo, kutokana na mwingiliano wa mataifa mbalimbali duniani," alisema.

Alisema, kwa kutambua ukweli huo, shirika lake nalo limeona kuna haja ya kushiriki katika vita dhidi ya ugonjwa huo kwa kuhimiza umma wa Watanzania kuchukua tahadhari kwa kuwa Tanzania si kisiwa kisichofikiana na wetu.

Diana alisema, shirika lake linatambua upotoshaji kuhusu chanjo na kusababisha baadhi ya watu kuzembea kupata huduma hiyo na kuongeza kuwa ni vyema kuendelea kuhimiza jamii kuchukua tahadhari.

Akipokea dozi milioni moja za chanjo aina mpya ya Sinovac, kati ya dozi milioni nne kutoka Uturuki juzi, Ummy alisema serikali ya Marekani imetoa msaada wa Sh. bilioni 57 kwa ajili ya mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Alifafanua kuwa serikali itatumia mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali kuendesha kampeni za chanjo katika mikoa 16 ili kufikia asilimia 70 ya Watanzania, watu wengi wachanjwe ili kusaidia kupunguza madhara ya ugonjwa huo pale kirusi kipya kitakapothibitika kuwapo nchini.




Mkuu wa Huduma za Bima Kitengo cha Benki (Bancassurance) wa kampuni ya Bima ya Maisha ya Sanlam Life Insurance, Krispinana Shirima (kulia), na Mkuu wa Uendeshaji wa kampuni ya Bima ya Maisha ya Sanlam, Tullo Mafuru (wapili kulia), wakikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 3.5 kwa familia ya marehemu ambaye alikuwa ni mnufaika wa huduma ya bima ya Maisha ya Elimu inayotolewa kupitia Benki ya CRDB. Wengine ni mtaalamu wa masuala ya bima kutoka benki hiyo, Wilbert Mweiro (wapili kushoto), Sango Rajabu Maundo mjane wa marehemu (katikati) na mtoto wake Paul Robert (kushoto). **MPIGAPICHA WETU**

# Chanzo ukatili kijinsia kwa familia hiki

**Na Christina Mwakangale**

IMEELEZWA kwamba kukithiri kwa matukio ya ukatili wa kijinsia katika jamii ikiwamo mauaji yanayosababishwa na malezi yasiyofaa wakati wa makuzi ya watoto kwenye familia na kuwafanya kukosa maadili na hofu ya Mungu.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Oliver Njogopa, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, akifungua mkutano wa kutathmini masuala ya kijinsia na ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Oliver alibainisha kwamba, kutokana na hali hiyo serikali imeanzisha programu ya malezi na makuzi jumuishi iliyozinduliwa Desemba mwaka jana, maalumu kwa ajili ya watoto kuanzia umri 0 hadi miaka nane, ikilenga mambo muhimu matano.

Alisema programu hiyo inajikita kwenye afya, lishe bora, malezi, ujifunzaji wa awali, ulinzi na usalama ili kuwekeza kwa watoto ambao bado ubongo wao haujaingiza vitu vingi kichwani.

Kuna changamoto kubwa ya malezi na makuzi, vitengo vingi vinavyoonekana sasa ni matokeo ya malezi ututoni na kuwafanya wasiwe na hofu ya Mungu. Tunawekeza kwa watoto hawa ili kuangalia maadili kwa kuwajenga walio katika umri huu," alisema Oliver.

Alisema pia kwa kipindi cha mwaka mmoja wa Raia Samia madarakani, yapo masuala muhimu ambayo yamepewa kipaumbele kwa ajili ya watu wenye ulemavu ikiwamo ujenzi wa shule za bweni 50 zilizo na vifaa saidizi kwenye halmashauri 50 zilizogharimu Sh. milioni 770 pamoja na kufufuliwa vyuo vya elimu na ujuzi. Pia Oliver alibainisha masuala mengine ambayo ni uwezeshwaji wa mikopo kwa watu wenye ulemavu kwa bajeti kutengwa ya Sh. bilioni tano kwa ajili ya ujenzi wa vibanda vya biashara kwenye majiji sita.

"Hadi Juni 30, mwaka 2021, katika fedha Sh. bilioni 53 za mikopo kwa vikundi 4,635 vilivyopata mkopo kati ya hivyo 761 vya watu wenye ulemavu pia vilinufaika na mkopo kwa kupata Sh. bilioni 9.1 kati ya fedha hizo," alisema Oliver.

Oliver alisema pia katika kipindi cha mwaka mmoja, kwenye mpango wa kutambua mapema watoto wenye ulemavu kwa kupata afua na utengamano, ilibainika watoto 28,698 katika kata 3,785 wana mahitaji maalumu ila tatizo ni kufichwa ndani na walezi au wazazi wao.

Meneja Uwezeshaji kutoka Asasi ya Foundation for Civil Society (FCS), Edna Chilimo, alisema mkutano huo uliondaliwa na ushirikiano wa asasi tatu ikiwamo Her-Ability, Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) na FCS, lengo ni kutambua mwezi Machi ambao ni maalumu kwa wanawake.

"Ndani ya mwezi huu wa wanawake FCS, SHIVYAWATA na Her-Ability ni kuangazia tathmini ya masuala ya jinsia pamoja na ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu ndani ya mwaka mmoja wa Rais Samia," alisema Edna.

## 30 wanyakua mil. 90/- za MastaBata

**Na Cristina Mwakangale**

WATANZANIA 30 ambao ni wateja wa Benki ya NMB, wamejinyakulia kitita cha Sh. milioni 90 huku kila mmoja akijipatia shilingi milioni tatu kupitia kampeni ya 'NMB MastaBata – Kivyako Vyako.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara kutoka benki hiyo, Filbert Mponzi, aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam, kufunga kampeni hiyo iliyodumu kwa miezi mitatu na kukamilisha kinyang'anyiro kilichobeba zawadi ya Sh. milioni 240.

Alisema malengo ya kampeni hiyo, kwa miezi mitatu iliyoendeshwa na benki hiyo, imefikia tamati Machi 23, mwaka huu, wamepewa wito wa kufungua akaunti benki ya NMB, kujihakikishia usalama wa fedha zao ikiwamo kunufaika na fursa za kibenki ikiwamo motisha mbalimbali.

Pia alisema kampeni hiyo, ilihamasisha matumizi ya kadi badala ya pesa taslimu na kwamba yamefanikiwa kwa kiasi kikubwa na huo ni mwanzo wa ujio wa kampeni nyingine.

"Hitimisho 'Grand Finale' la kampeni hiyo, limefanyika NMB Tawi la Sinza jijini Dar es Salaam, kufikia ukomo kwa mchakato uliowanufaisha wateja 1,080, kati yao 1,000 wakijinyakulia Sh. milioni 100 huku 50 wakitwaa Sh. milioni 50 na 30 wa fainali wakishinda shilingi milioni 90.

"Kampeni ilianza Desemba mwaka jana, ikilenga kuhamasisha wateja kutumia kadi katika kufanya malipo. Matumizi ya pesa taslimu yapo, ila tunapaswa kuyapunguza kwa sababu za kiusalama. Tunatumia nguvu kubwa katika kuhamasisha wateja kutumia kadi za MasterCard kufanya malipo yoyote, bila kuwa na pesa taslimu," alisema Mponzi na kuongea:

Pesa zilizotolewa kwa wateja ni kama motisha yetu kwao, kwamba wamefanya manunuzi kwa faida zao wenyewe, sisi kama benki tukaona tuwazawadie katika kuchagiza matumizi yasiyohusisha pesa taslimu."

Aliongeza kwamba kampeni hazijakoma, zitaendelea kwa kutoa elimu kwa jamii kutambua umuhimu wa mabadiliko, kwa sababu matumizi ya kadi ni rahisi, nafuu na salama zaidi akisema imekuwa na mafanikio na kumekuwa na ongezeko la asilimia 10 la watumiaji wa kadi.

Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Elibariki Sengasenga, alipongeza aina ya ushirikiano kati ya NMB na bodi yake, tangu kuanza kwa kampeni hiyo Desemba mwaka jana walipoenda kwao kuomba leseni ya kuendesha droo za kampeni hiyo.


"Pongezi kwenu NMB kwa kufuata taratibu, kuja kwetu kuomba leseni ya kuendesha kampeni hii na kila droo mkahakikisha kunakuwa na mwakilishi wetu. Kwa kipindi chote, hatukupokea malalamiko yoyote. Ilikuwa ni kampeni rahisi kwa mteja kushiriki, ile kufanya tu matumizi yako mwenyewe na kwa faida zako, unajikuta katika nafasi ya kuzawadiwa.

"Na jambo la kufurahisha zaidi, idadi ya washindi ilikuwa ni kubwa mno, hivyo wanufaika walikuwa wengi. Mngeweza kubuni shindano dogo lenye kuwazawadia wateja wachache, ila mkaona hapana, mufaikie wengi zaidi, hili ni jambo la kupongezwa," alisema Sengasenga.




Ukurasa 12

Mradi uboreshaji Dar unavyofungua mkoa katika kona zake zote




Ukurasa 13

Tulieni dawa ya sindano ya Hangaya iingie!

BUFE
IJUMAA MACHI 25, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

**Wizara ya Fedha: Kukopa ni zao la vipaumbele, haihusu awamu**

# Wajue wenye ulemavu wanaounda jiko la kisasa litunzalo mazingira

## • Ni kikundi, malighafi asili, teknolojia juu

**Na Amri Lugungulo,** Kisarawe



Iddi Kinega, mjasiriamali na mbunifu wa mradi wa kutengeneza majiko, akiwa kazini kwake Kisarawe. **PICHA: AMRI LUGUNGULO**

IDDI Saidi Kinega (50) ni mkazi wa kijiji cha Homboza, katika kata ya Msimbu, wilayani Kisarawe, mkoa wa Pwani ameanzisha mradi wa kiwanda cha kutengeneza majiko sanifu yanayotumia nishati ya asili ikiwamo ya mkaa, kuni na pumba ya mbao zikitumika kiasi kidogo kufanyia upishi na shughuli nyingine zinazohitaji nishati hiyo.

Kinega ambaye ni mlemavu wa viungo, pia ni Mwenyekiti wa kikundi cha Tupendane Walemavu, anafafanua kwamba kikundi chake ndicho kinachomiliki mradi huo wa utengenezaji majiko sanifu.

Anasema ameanzisha mradi kwa nia ya kupambana na umasikini na kupambana na uharibifu wa mazingira ya misitu.

Mjasiriamali huyo, aliyezaliwa mwaka 1972 na kupata elimu ya shule ya msingi hadi darasa la saba kijijini humo, anasema wanamiliki kiwanda hicho kidogo cha kutengeneza majiko hadi yenye uwezo wa kupika chakula cha kilo zisizopungua ishirini kwa mpigo.

Mradi huo ulianzishwa mwaka 1997 katika kijiji hicho jirani na jiji la Dar es Salaam, upo kando ya njia panda ya barabara iendayo kijiji cha jirani cha Msanga Zalala hadi Masaki na barabara ya kwenda Shule ya Msingi ya Homboza na zahanati ya kijiji hicho.

Uzalishaji wa majiko hayo sanifu, unafanywa na mafundi wa kukodi kutoka nje wanachama wengine wakiwamo katibu, mweka hazina na wajumbe wawili wa kikundi hicho cha Tupendane Walemavu, siyo mafundi, bali mwenyekiti na mafundi wa kukodi hufanya kazi hizo.

Mafundi hao wa kukodi hulipwa posho zao baada ya kutengeneza majiko, kulingana na maendeleo yanayopatikana na Kinega anasema ameshaanza kunufaika yeye na wanachama wenzake.

"Mimi nimeweza kujenga nyumba na kusomesha watoto wangu shule ya msingi na niliweza kupata milo yangu ya kila siku isiyopungua mitatu, ikiwemo ya asubuhi, mchana na jioni na kumudu gharama nyingine ndogondogo zikiwemo za matibabu," anasema

Mwenyekiti huyo anafafanua kuwa, mradi huo ambao ni wa kifamilia umemuondolea bughudha ya kuwa tegemezi kwa watu wengine badala yake yeye ndiye sasa anayetegemewa.

Vivo hivyo, anasema kuwa hata kwa wanachama wenzake wamenufaika kwa kupata mahitaji yao ya kila siku yakiwemo chakula.

Mjasiriamali huyo anaeleza manufaa mengine, kwamba majiko yamempunguzia gharama na hata uharibifu wa mazingira, malighafi zake zinapatikana kijijini, ikiwamo udongo wa mfinyanzi, huku mabati na saruji yakipatikana kutoka jijini Dar es Salaam, ambako ni jirani.

Anaeleza kwamba majiko hayo sanifu yanayotumia nishati ya asili yanapambana na uharibifu huo wa mazingira pia hupunguza gharama za kupikia kwani hutumia kiasi kidogo tu cha nishati hizo asili.

Kinega anasema sasa anakusudia kukuza kiwanda hicho kwa kuweka mashine za kusaidia matengenezo, ili azalishe bidhaaa hizo kwa wingi na bora zaidi, kuliko sasa inatumika mikono na nguvu nyingi kuzalisha bidhaa hivyo inafanya kazi kuwa ngumu.

# Mradi uboreshaji Dar unavyofungua mkoa katika himaya zake zote

**Na Mwandishi Wetu**



Kituo cha Afya Buza kilichopo katika kata ya Buza, Manispaa ya Temeke. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

"KIJICHI ya leo, ni tofauti sana na Kijichi ya miaka ya nyuma. Mitaa ilikuwa mibovu na mifereji ya kupitishia maji machafu ndio ilikuwa balaa kipindi cha mvua. Maji yanaingia hadi kwenye majumba ya watu. Lakini kwa sasa Kijichi ni Ulaya," anasema Mwantumu Hussein, mkazi wa Mtoni Kijichi wilayani Temeke, Dar es Salaam.

Dereva wa bodaboda katika kona ya Neluka, Mtoni Kijichi, Lucas Mauma, anasema ujenzi wa barabara katika mitaa ya Mtoni Kijichi umerahisisha sana shughuli yao ya kusafirisha abiria katika maeneo mbalimbali.

"Kabla ya ujenzi wa hizi barabara kwa kiwango cha lami kazi yetu ilikuwa ngumu kidogo lakini sasa unateleza tu. Lami hizi pia zimependisha hadhi ya Kijichi. Licha ya kupanda bei, siku hizi pia kupata chumba Kijichi si rahisi," anasema Mauma.

Kijichi ni kati ya maeneo kadhaa ya Jiji la Dar ambayo yameboreshwa sana kutokana na Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam au 'Dar es Salaam Metropolitan Development Project - DMDP'.

### MRATIBU WA MRADI

Mratibu wa Mradi huo ulioko chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Humphrey Kanyenye, anasema mradi huo unatekelezwa kwa fedha za Benki ya Dunia ulibuniwa ili kutekeleza mambo matatu.

Anasema mradi ulilenga kuboresha huduma za jamii kama miundombinu na kujenga uwezo wa Manispaa za Jiji la Dar es Salaam katika utoaji huduma na kuchangia katika kukabili changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Lengo la tatu, anasema ni kusaidia kukabili matukio makubwa ya dharura kama majanga yanayoweza kuukuta mkoa wa Dar es Salaam.

Anasema serikali iliamua kutekeleza mradi huo kwa kuangalia Dar es Salaam katika hali ya upekee, kutokana na jiji hilo linalokua kwa kasi, kukadiriwa kuwa na idadi ya wakazi zaidi ya milioni 10 ifikapo mwaka 2030.

Lingine lililoangaliwa, Kanyenye anasema, Dar es Salaam inakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiutawala katika kuwajibikia vyema wakazi wake.

Msingi wake ni kwamba, Manispaa za mkoa zilihitaji nyenzo muhimu za ukusanyaji mapato ya ndani, ili kupunguza utegemezi wa serikali kuu katika mipango

> **"Utaona kwamba, kutokana na ukuaji wa kasi wa jiji sambamba na mabadiliko ya tabianchi, athari za mafuriko zilitarajiwa pia kuongezeka.**


Mradi wa Stendi Mpya ya Kinyerezi iliyopo katika wilaya ya Ilala ukiwa umekamilika.

na bajeti zake.

"Ukuaji wa Jiji (mkoa) la Dar es Salaam unakabiliwa na makazi yasiyopimwa kwa kati ya asilimia 70 mpaka 80. Kutokana na ukuaji kasi wa Jiji la Dar es Salaam na mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili dunia, athari za mafuriko zinatarajiwa kuongezeka Dar es Salaam. Hivyo, bila kuwa na mipango bora ya utoaji wa huduma, jiji hili linaweza kutokalika au kutotawaliwa.

"Utaona kwamba, kutokana na ukuaji wa kasi wa jiji sambamba na mabadiliko ya tabianchi, athari za mafuriko zilitarajiwa pia kuongezeka," anasema.

Anasema bila kuwa na mipango bora ya utoaji huduma, Dar es Salaam inaweza kufikia hatua haikaliki.

Kanyenye anasema, mradi DMDP ulianza rasmi mwaka 2016 huku awamu ya kwanza ikikamilika mwaka 2020, unahusisha ujenzi wa barabara za lami sambamba na mifereji ya maji taka, uwekaji wa taa za barabarani za sola pamoja na madaraja.

Anafafanua kuwa mradi pia unahusisha ujenzi wa masoko ya kisasa yakiwa na huduma za kibenki na maeneo ya umma ya kupumzikia, ukarabati wa viwanja vya michezo na ujenzi wa vyoo vya umma.

Mratibu Mradi huyo, anasema kabla ya kuanza mradi huo, ulifanyika usanifu na kufuatwa vigezo muhimu, maeneo ya watu wenye kipato cha chini na yaliyojengwa kiholela yakitiliwa maanani, ili kuunganisha wilaya zote za mkoa.

"Mradi huu una thamani ya Dola za Marekani milioni 300 (Sh. bilioni 660). Sio fedha hizo tu tulizopata kwa ajili ya mradi, bali tumepata pia Dola za Marekani milioni tano (Sh. trilioni 11) kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Nchi za Nordic (NDF) kwa ajili ya kukabili changamoto za mabadiliko ya tabianchi na serikali ya Tanzania ina changia Dola za Marekani milioni 25.3," anasema.

Anafafanua kuwa, fedha hizo zimegawanywa katika manispaa zote za jiji ambazo zitajenga barabara za kati (feeder roads) zenye urefu wa kilometa 65.6, ujenzi wa mitaro mikubwa yenye urefu wa kilometa 31.8 na barabara za mitaa kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 145.0.

Mkelewe Tungaraza, Mratibu wa Mradi wa DMDP katika Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni, anasema ujenzi wa miundombinu unaendelea vizuri na kwamba mpaka sasa kuna barabara zimeshakamilika kama vile barabara za kuzunguka stendi za Makumbusho na Shekilango, Sinza.

"Tunataka mtu akiwa Dar es Salaam aweze kuchepuka kwenda barabara nyingine, ili kupunguza foleni katika barabara kuu. Vilevile, taa zitakazojengwa katika barabara hizo zitaimarisha usalama," anasema Tungaraza.

Anasema, barabara zinajengwa na mifereji ya maji ya mvua na madaraja kwa maeneo sumbufu, lengo ni kuzuia mafuriko.

Tungaraza anataja maeneo yanayojengwa vyoo vya umma kwa Wilaya ya Kinondoni, ni zilizopo Tandale, Mburahati na Mwananyamala.

### MABOSI TARURA

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) Wilaya ya Temeke, Paul Mhere anasema mradi wa DMDP katika Manispaa ya Temeke, umetekelezwa katika kata 16 kati ya 23 zilizopo.

Anasema unahusisha upimaji viwanja 800 vya mfano wa upangaji miji, ujenzi wa mtandao wa barabara za lami (zaidi ya kilomita 84) na uwekaji taa za barabarani katika kata saba.

Ni ujenzi anaosema umehusisha pia masoko ya kisasa manne katika kata za Kilakala, Yombo, Vituka, Kijichi na Mbagala Kuu.

Vivyo hivyo, mradi umehusisha uboreshaji zahanati ya Makangarawe, ujenzi wa vituo vya mabasi vinne katika kata za Kilakala, Kijichi, Yombo Vituka na Mbagala Kuu, vyote katika wilaya ya Temeke.

"Tumejenga pia mifereji ya maji ya mvua na mabwawa ya kukusanyia maji ya mvua ili kupunguza athari za mafuriko. Tumeboresha pia mfumo wa utawala, ukusanyaji wa mapato na mipango ya maendeleo ya halmashauri," anasema.

Mhere anasema kumekuwapo malipo ya fidia jumla Sh. Bilioni 20 na uboreshaji mfumo wa ukusanyaji taka ngumu katika maeneo hayo. Meneja wa Tarura Wilaya ya Ilala, Silvester Chinengo, anasema katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, miradi iliyotekelezwa ni ujenzi wa barabara za Ndanda, Olympio, Kiungani, Omari Londo na Mbaruku zenye urefu wa kilomita 3.265.

Pia, anasema kumefanyika ujenzi wa jengo la ghorofa moja la ofisi na maabara ya mradi, ujenzi wa mifereji ya Bonde la Mto Msimbazi wenye urefu kilomita 6.1 na ujenzi wa mfereji wa Bonde la Mto Yombo, kilomita 9.82.

Chinengo anasema, mradi pia umehusisha ujenzi wa barabara za lami kilomita 7.78, vizimba vya kukusanya taka ngumu vinne katika kata ya Gongolamboto, pamoja ujenzi wa barabara (Kilomita 12.049).

Katika kata ya Kiwalani, anasema ujenzi umehusisha masoko, mifereji ya maji ya mvua kilomita tatu, ujenzi wa vyoo vitatu na uchimbaji visima virefu viwili.

Pia, mradi unatajwa umehusisha ujenzi wa Soko la Bombom katika kata ya Kiwalani, barabara ya Ulongoni B - Bangulo - Kinyerezi (Km 7.5), Ujenzi wa Daraja la Ulongoni B na stendi ya daladala ya Kinyerezi.

### UONGOZI MTAA


Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kijichi, Anaclet Hayuka, anasema soko lililojengwa Mtoni Kijichi, litakuwa na huduma zote muhimu pamoja na ofisi za maofisa afya ili kufanya ukaguzi wa bidhaa kila mara.

Mfanyabishara wa duka la nguo pembezoni mwa barabara ya kuingia kituo cha Makumbusho, Jamila Okamu (34), anasema kujengwa kwa barabara hiyo kumeboresha biashara zao na kuwaongezea fursa.

Awali, anasema walipata shida ya vumbi kutokana na ubovu wa barabara na kwamba wateja wenye magari walishindwa kusimama kununua bidhaa kwenye maduka yao.

Mradi huo umetekelezwa kupitia fedha za Mradi wa Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam yaani (DMDP) wa awamu ya kwanza unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

## TAFAKURI YA MLALAHOI




# Tulieni dawa ya sindano ya Hangaya iingie!


NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

HII nchi ukiniambia nihame unatwanga maji kwenye kinu, yatakumwagikia tu. Hasa wakati huu ambao nchi inaelekea kupona na kutulia kama zamani, hata aje yule aliyesema tuhamie Burundi, yatamlowesha tu.

Nakumbuka kuna mwingine mwaka fulani hivi akaibuka na kutwambia kuwa wale wakazi wa Dar es Salaam kama kuna mtu atapindukia mwezi Julai mwaka huo, bila kurudi kijijini atakuwa mwanamume wa shoka. Kweli wanaume tukakaza na tukabaki jijini.

Nchi hii ina mambo mengi ya kuvutia na kuvutiwa, usipokaa sawa itakuacha na kubaki unatoa macho kama mjusi aliyebanwa mlango. Kuna watu wa aina mbalimbali wanaoeleweka na wasioeleweka, wajulikanao na wasiojulikana.

Hebu fikiria mtu mmesoma wote msingi mpaka sekondari, mkaachana huko juu na mkaja kukutana nchi imerejea katika mfumo wa siasa ya vyama vingi. Mtu huyo anakukuta huvai shati kijani bali ya rangi zingine, anakushangaa na kukuona adui.

Anakumbuka jinsi mkiwa msingi mlivyokuwa chipukizi wa kuvaa shati kijani na kaptula nyeusi, eti anakushangaa leo unavaa shati jekundu na suruali buluu anakutazama kwa jicho jekundu! Unamuuliza, anakwambia umepotea.

Nitapoteaje wakati nimo nchi hii hii ya Nyerere? Anasahau kuwa hata wazazi wako walipigania Uhuru wakiwa na Nyerere na kina Kawawa, wakivaa mashati yaliyofanana. Leo wewe kutafuta mawazo mengine anakuona adui zuzu!

Ni kama wale waliomtazama jicho jekundu Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan mwaka 2017 alipokwenda Nairobi, Kenya kumjulia hali Tundu Lissu na wakamtazama jicho jekundu Joseph Sokoine alipofanya hivyo hivyo Ubelgiji!

Ni watu wa mazoea hawa. Wanaomtazama jicho jekundu Chifu Hangaya aliposhikana mkono na Lissu pale Brussels na kumtaza hivyo hivyo alipomwita Freeman Mbowe pale Ikulu ya Dar es Salaam na kuzungumza naye!

Watu wa mazoea hawa ambao walikuwa wakisikiliza na kuamini kwamba aliko mpinzani hakupaswi kupelekwa maendeleo, wakidhani pengine mpinzani aliumbwa na nini vile, huku mtawala akiumbwa na Mungu! Watu wa ajabu hawa.

Huenda ndio hao hao waliowatazama kwa macho mekundu viongozi wa dini walipomwomba Rais Samia kuangalia mustakabali wa kesi ya Mbowe na kina Adamoo na hatimaye DPP ambaye pia walimwangalia kwa macho pilipili kichaa, aliposema hana nia ya kuendelea nayo.

Hebu Watanzania tukae chini tufikirie, hivi nchi hii ni ya nani na watu wanaoishi ndani yake ni ndugu za kina nani? Mnashindwa kukaa chini na kujiuliza kuwa sisi sote ni wana wa Adamu (Si Adamoo) na ndiyo sababu tukaitwa bin-Adamu!?

Chifu Hangaya halali akifikiria jinsi ya kuwaleta Watanzania pamoja kama walivyopata kuwa huko nyuma kabla ya kuvurugana kisiasa uchwara hapa katikati, siasa ambazo zilitaka kuaminishwa kuwa zinajengwa kwa utengamano. Mama huyu ambaye hata kwa kumwangalia tu unaona kweli akifanyacho ni cha rohoni na si cha usoni, anajitosa licha ya kutazamwa kwa macho makali, anakutana na wanasiasa wa upinzani anakaa nao mezani na kujadili mustakabali wa nchi.

Tunakaa pembeni kumsema hasa, kana kwamba nchi hii imeumbiwa rangi moja tu jamani! Haya sasa je na hao wengine wakiibuka wakasema uchumi wa buluu ni wa nini, mtasemaje?

Upinzani kwa wanaoujua vizuri na kuutumia inavyopaswa si uadui, kwamba ukishakaa kambi hiyo basi hufai tena kuwa Mtanzania au mwananchi, asiyestahili hata!

Hivi kama Chifu Hangaya hicho kidogo anachokitafuta majuu huko na kukileta nchini, angefika na kusema hiki kitakuwa ni kwa ajili ya waamini wa kijani tu na si wa buluu au bulaki ingekuwaje?

Hivi angejuaje kuwa shule au madarasa yale yanayojengwa yatatumiwa na wa kijani tu, au barabara ile itapitwa na wa kijani tu, au kituo kile cha afya watadungwa sindano wale wa kijani tu, tungekuwa wapi?

Polepole sindano ya Dokta Hangaya inaingia, hivyo tulieni dawa iingie, dawa itakayoleta maridhiano na Watanzania wakarejesha upendo na mshikamano wao kama zamani. Hivyo wale wa mazoea tulizeni panapodungwa ili msivunje sindano ya Dokta mambo yakaharibika. Alamsiki!

FEDHA

# Wizara ya Fedha: Kukopa ni zao la vipaumbele, haihusu awamu

• Wenye dhamana wasisitiza linalipika

**Na Mwandishi Wetu**

KUMEKUWAPO na mitazamo inayokinzana nchini miongoni mwa wananchi kuhusiana na suala la deni la taifa husussan serikali inapokopa nje huku ikiendelea kudaiwa madeni ya nyuma.

Hoja hii imekuwa na mjadala mkubwa miaka ya sasa, kutokana na watu kadhaa katika jamii kulizungumzia kwa mitazamo tofauti hususan wanasiasa bila kuwaelimisha wananchi ambao hawana uelewa wa masuala ya uchumi kuhusu maana halisi ya deni la taifa na sababu za nchi kukopa.

Kutokana na wananchi wengi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na hilo, wamekuwa wakilipokea na kulipa tafsiri mbalimbali, ikiwamo kuamini kuwa nchi kukopa na kushindwa kulipa kunaweza kusababisha ifilisiwe na tafsiri nyingine nyingi.

Wapo watu wanaosema kuwa deni la taifa linagawanywa kwa idadi ya watu, ili kuonyesha kuwa kila Mtanzania anadaiwa, hivyo kusababisha upotoshaji unaoibua taharuki kwamba serikali inakopakopa bila kuzingatia vipaumbele na bila kuwapo utaratibu wala mifumo ya udhibiti na kulifuatilia.

Aidha, kukosekana kwa uelewa kumekuwa kukisababisha baadhi ya watu kuzilinganisha awamu za uongozi katika suala la kukopa; kwamba awamu fulani ilikopa sana na nyingine ilikopa kidogo.

Kimsingi, nchi zote duniani zikiwamo tajiri na zenye viwanda hukopa kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo. Sababu kubwa inayoisukuma nchi kukopa ni kutokana na kuwa na nakisi (upungufu wa fedha) katika kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya bajeti ya mwaka husika.

Kwa mfano, mwaka ujao wa fedha wa 2022/23 ukomo wa bajeti ya Tanzania ni shilingi trilioni 41.063, lakini wakati wa utekelezaji utakapoanza kuanzia Julai Mosi bila fedha zinazotarajiwa kuwa pungufu katika vyanzo vya mapato, hakutakuwa na njia nyingine zaidi ya serikali kukopa.

Kitu kingine ambacho wananchi wengi hawakielewi ni kwamba deni la taifa halitokani na deni la serikali pekee bali linajumuisha pia deni la sekta binafsi.



Kamishna wa Madeni anayesimamia Deni la Taifa, Japhet Justine **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba

> **"Kitu kingine ambacho wananchi wengi hawakielewi ni kwamba deni la taifa halitokani na deni la serikali pekee bali linajumuisha pia deni la sekta binafsi.**

### KAMISHNA WA MADENI

Kamishna wa Madeni anayesimamia Deni la Taifa katika Wizara ya Fedha na Mipango, Japhet Justine, anaeleza kwamba sekta binafsi kwa kuwa inakopa nje fedha za kigeni, kisheria madeni hayo yanapaswa kusajiliwa katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT), zikiwa ni jitihada za kufuatilia mwenendo wake kama sehemu ya deni la Taifa, huku akisema baadhi ya sababu za kukopa nje ni kuzuia mtikisiko wa shilingi, kuongeza kiasi cha fedha za nje na kufungua fursa.

Kufungua fursa ni kutekeleza miradi mikubwa ikiwamo ya kimkakati inayoendelea kujengwa nchini kama ya umeme, reli, barabara, bomba la mafuta na mingine ambayo haiwezi kutekelezwa kama nchi inaogopa kuwa na deni la taifa.

Justine ambaye aliwasilisha mada katika mafunzo ya waharisi wa vyombo vya habari kuhusu Deni la Taifa wiki iliyopita jijini Arusha, anasema kwamba zipo taratibu mbalimbali zinazofuatwa kuhakikisha kwamba deni hilo linaendelea kuwa himilivu ili taifa kuendelea kukopesheka.

Anatoa mfano, kwamba Wizara ya Fedha na Mipango haiwezi kukopa katika benki za nje na taasisi za fedha duniani, zikiwamo Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa ( IMF) bila kuangalia muundo wa bajeti wa mwaka husika na kwamba mikopo isizidi asilimia tano ya bajeti.

### MIKOPO INAVYOIBULIWA

Naibu Kamishna wa Madeni anayesimamia Deni la Taifa katika Wizara ya Fedha na Mipango, Noor Ndile, anasema kwa utaratibu uliowekwa na serikali, haiwezekani Deni la Taifa kuleta shida, kwa kuwa mifumo iliyoko ya uratibu inajitosheleza.

Anasema kamati zilizopo katika kupitia mikopo ya nje hakuna kitu chochote kisichozingatia maslahi ya umma kinaweza kupenyezwa na kuifanya nchi ikope fedha. Kamati hizo zinaanzia na kuibua miradi ndani ya wizara husika, taasisi au wakala wa serikali. Baada ya kamati hiyo kuwasilisha mradi inaotaka kuutekeleza maombi yanapelekwa kamati ya pili ya wataalamu wa madeni katika Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi na baada ya kupitia vigezo vyote na kujiridhisha inaupeleka kamati ya kitaifa ya kumshauri Waziri wa Fedha na Mipango.

Kamati ya Taifa inaundwa na Katibu Mkuu Hazina, Katibu Mkuu Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) Zanzibar, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar na Gavana wa BoT.

Kamati hii baada ya kupitia, kushauriana na kupitisha hupeleka Idara ya Mipango kwa ajili ya kuanza mchakato wa maombi ya mkopo.

Kuhusu kamati ya kitaifa kuijumuisha Zanzibar, Justine, anaeleza kwamba hilo linatokana na Zanzibar kuwa sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na linapokuja suala la mikopo zinakopa pamoja.

Justine anasema kutokana na utaratibu huo mzuri wa kuwa na kamati za kushughulikia mikopo ya nje, hakuna dalali yeyote anayeweza kufanikiwa kujipenyeza na kufanikisha malengo yake binafsi ya kujinufaisha, yakiwamo ya kudai kuwa atasaidia kufanikisha upatikanaji wa mkopo, na kwamba hizo ndizo taratibu zinazolifanya Deni la Taifa kuendelea kuwa himilivu.

Justine na Ndile kwa pamoja wanaweka msisitizo kuwa suala la kukopa halina uhusiano wowote na awamu za uongozi tangu ya kwanza hadi ya sita, kwa kuwa fedha hizo hazikukopwa na kiongozi husika bali zilikopwa kwa kuzingatia vipaumbele vya wakati ule na ndio maana madeni ya miaka mingi iliyopita yanalipwa sasa.

### WENYE DHAMANA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, anawaondolea Watanzania hofu ya nchi kushindwa kulipa Deni la Taifa kwa kusema serikali imejiwekea utaratibu mzuri wa kulipa kila tarehe inapofika.

"Hatuna nia ya kukwepa kulipa deni sisi kama taifa huru, nchi yetu ni tajiri ndio maana tunakopeshwa na Benki ya Dunia na IMF. Ndio maana wanatuamini baada ya kufanya tathmini yao."

Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, akiwasilisha mapendekezo ya serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka huo kwa wabunge jijini Dodoma Machi 11, mwaka huu, alisema hadi Desemba 2021, Deni la Taifa lilikuwa Sh. trilioni 68.52 kutoka Sh. trilioni 58.68 kwa kipindi kama hicho mwaka 2020, huku akisema bado ni himilivu.

Mjadala kuhusu Deni la Taifa ni muhimu kwa nchi, lakini ili ujielekeze katika uhalisia bila kutanguliza mbele maslahi binafsi badala yake kutanguliza maslahi ya Taifa, ipo haja kwa serikali kuendelea kuwatumia wataalamu wake kutoa elimu kwa makundi kadhaa ya jamii, wakiwamo wanasiasa, akisisitiza elimu hiyo itasaidia kupunguza upotoshaji kuhusu dhana nzima ya Deni la Taifa.



## Samia aipaisha Tanzania kiutalii

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

PROGRAMU ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutangaza utalii ujulikanao Royal Tour imeifanya Tanzania kuwa kivutio cha kwanza cha utalii Afrika mwaka 2022, huku ikivuta wawekezaji mbalimbali.

Miongoni mwa wawekezaji waliovutiwa kuwekeza Tanzania baada ya kuona programu hiyo ni wawekezaji kutoka taifa la Bulgaria ambao wanakusudia kujenga malazi yenye hadhi ya kimataifa kwenye hifadhi mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo kuhusu mafanikio ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Waziri Dk. Damas Ndumbaro, alisema kupitia programu hiyo mtandao maarufu wa habari nchini Marekani 'theGrio' umetambua juhudi za Rais katika kuongoza vyema sekta ya utalii nchini imeipaisha Tanzania.

"Programu hii kwa ujumla imeanza kuleta matunda kwa kuvutia watalii na wawekezaji mbalimbali kuja nchini, mathalan wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka nchi masoko ya utalii yakiwamo Marekani, Ufaransa na Lithuania wamehamasika kutembelea nchini ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema wawekezaji wa Bulgaria watajenga malazi hayo yenye hadhi ya nyota tano zitakazoendeshwa na Kampuni ya Kempiski katika Hifadhi ya Taifa za Serengeti, Manyara, Tarangire na Ngorongoro.

Alisema hatua hiyo italeta matokeo chanya katika kuongeza idadi ya vyumba na wigo wa mnyororo wa huduma kwenye sekta ya utalii.

Kadhalika, alisema pamoja na uwapo wa ugonjwa wa UVIKO -19 ambao uliathiri sekta hiyo watalii wa nje, waliotembelea vivutio wameongezeka kutoka 620,867 kwa mwaka 2020 hadi watalii 922,692 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 48.6.

"Pia mapato ya watalii wa kimataifa yanakadiriwa kuongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020, hadi Dola za Marekani milioni 1,254.4 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 76," alisema.

Akizungumzia kuhusu watalii wa ndani, alisema idadi yao iliongezeka kutoka watalii 562,549 mwaka 2020 hadi 788,933 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 40.2 huku mapato yakiongezeka kutoka Sh. bilioni 9.7 mwaka 2020 hadi Sh. bilioni 12.4 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 27.8.

Alisema maboresho yaliyofanywa kwenye sekta hiyo yameipa Tanzania tuzo za kimataifa ikiwamo kutambuliwa na heshima ya kushiriki kuwa mwenyeji wa matukio mbalimbali.

# Sababu ongezeko ukatili kingono vyuoni yaanikwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema kuchelewa kuanzishwa kwa madawati ya jinsia kwenye vyuo vya elimu ya juu na kati unachangia ongezeko la vitendo vya ukatili wa kingono.

Dk. Gwajima alibainisha hilo wakati akifungua kikao cha kwanza cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo kilichofanyika jijini hapo.

Alisema kumekuwa na kasi ndogo kuliko ilivyoelekezwa na serikali na kutaka kasi iongezwe katika uanzishwaji wa madawati hayo.

"Wizara iliandaa mwongozo na kuratibu uanzishwaji wa madawati haya kwa lengo la kuweka mfumo wa kushughulikia masuala ya unyanyasaji wa kingono na vitendo vya ukatili katika vyuo vya elimu ya juu na kati na kuimarisha ulinzi wa wanawake na watoto dhidi ya vitendo hivyo."

"Katika vyuo hivi nimefuatilia takwimu, kasi ya uanzishwaji wa madawati haya ni ndogo sana, hivi vyuo vilitakiwa vione umuhimu wa uwepo wa madawati haya, nadhani kuwe na mawasiliano kati ya baraza hili na mabaraza ya vyuo kuona sera ya usawa wa kijinsia katika vyuo inavyotekelezwa," alisema.

Waziri Gwajima alionyesha kusikitishwa pia na baadhi ya wafanyakazi wa vyuo kuwa vikwazo vya uanzishwaji wa madawati hayo kwa wao wenyewe kufanya unyanyasaji wa kijinsia.

Alibainisha serikali itahakikisha mwongozo huo unafika hadi katika shule za msingi na sekondari ili kusaidia mapambano ya kutokomeza ukatili wa kijinsia.

"Dunia yote kwa sasa inaelekea kwenye kuimarisha usawa wa kijinsia hasa kwenye masuala ya kiuchumi hivyo nitoe wito Watanzania kujipanga kupata fursa hizo kupitia kamati iliyoundwa kuratibu utekelezaji wa ahadi za nchi katika jukwaa la usawa wa kijinsia," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Zainab Chaula, alimhakikishia Waziri kuwa Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ili kutokomeza vitendo vya ukatili kwani ndiyo msingi katika kuimarisha usawa wa kijinsia.

Dk. Chaula alisema pamoja na vikwazo vilivyopo Wizara imejipanga kushughulikia ustawi na maendeleo ya jamii kwa makundi yote.

"Suala la ukatili wa kijinsia tumelishikia bango japo bado halijaongelewa vya kutosha, tutaendelea kwa kushirikiana na wadau. Vilevile kuhakikisha tunatatua changamoto ya uhaba wa watumishi, ukosefu wa ajira na uchakavu wa majengo hasa ya makazi ya wazee," alisema Dk. Chaula.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) katika Wizara hiyo, Ikusubisya Kasebele, alishukuru uongozi wa baraza hilo kwa kufuata sheria na kukaa vikao mara mbili kwa mwaka.



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Elirehema Kaaya (wapili kushoto), akiwa na wataalamu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wakikagua fremu za kuwekea biashara za mitumba, walipotembelea soko la wazi la wafanyabiashara wadogo maarufu machinga, Barabara ya Bahi, jijini humo jana.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wafugaji wapewa sharti kumiliki mashamba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka wafugaji kuhakikisha wanapima ardhi waliyonayo ili kupatiwa hati ya umiliki wa mashamba na kuepuka migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara.

Pia amewataka kuwa na ufugaji wenye tija kwa kufuga kisasa jambo litakalowasaidia kujikwamua kiuchumi wao na familia zao kupitia mifugo yao.

Mtaka aliyasema hayo jana, wakati akifungua mkutano kati ya wafugaji wa Mkoa wa Dodoma na viongozi wa mkoa, wenye lengo la kuwaelekeza juu ya umuhimu wa ushiriki wa sensa kwa wafugaji, pamoja na utambuzi wa mifugo.

Alisema ofisi yake itashirikiana na watu wa Idara ya Ardhi kutoa kipaumbele kwa wafugaji katika upimaji wa maeneo ili kuwa na hati miliki.

"Nakuelekeza mwenyekiti wa wafugaji nchini, waeleze wafugaji wako juu ya umuhimu wa kuwa na ardhi ambayo imepimwa, la sivyo wataendelea kusumbuka kila iitwapo leo kwa sababu ya kukwepa sheria ya umiliki ardhi," alisema Mtaka.

Alisema hivi sasa dunia inakwenda katika ufugaji wa kisasa wenye tija, hivyo ni vyema nao wakabadilika ili kuendana na wakati wa sasa, wapime mashamba yao ambayo yatawasaidia kutenga sehemu ya malisho ya mifugo.

"Ni wafugaji wachache sana ambao wana ng'ombe lakini hawana ardhi, hivyo hilo ni jambo la msingi, kuchukua hatua ya kupima ardhi mliokuwa nayo ili muwe salama," alisema Mtaka.

Alisema anahitaji kuona mfugaji anakuwa na bima ya afya, anasomesha watoto katika mazingira mazuri, anaishi sehemu nzuri kupitia ufugaji anaofanya.

Kuhusu uwekaji hereni kwenye ng'ombe, Mtaka alisema wafugaji wanapaswa kuondokana na dhana ya kupiga chapa ng'ombe kwa kutumia moto, badala yake wawavishe hereni ambazo zitawasaidia kufanya utambuzi wa mifugo waliokuwa nayo.

Alisema ng'ombe akiwekewa hereni hata akipotea ni rahisi kumpata kwa sababu tayari anakuwa kaingia katika mfumo wa utambuzi wa mifugo.

Alifafanua zaidi ya kuwa karne ya sasa kila kitu kwa mnyama kina thamani kuanzia ngozi ya ng'ombe hadi kwato zake.

"Jitahidini kuwavisha hereni mifugo yenu, itawasaidia kuitambua hata ikipotea kwenda sehemu nyingine," alisema Mtaka.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, aliwataka wafugaji kutumia elimu waliopata kuhusu ufugaji wa kisasa, ili kwenda kufanya mabadiliko ya ufugaji wanaofanya badala yake wafuge kwa tija.

Mfugaji kutoka Kongwa, Yared Yacob, aliushukuru uongozi wa mkoa kutokana na kuwapa elimu ya namna ya ufugaji wa kisasa, pamoja na kuwasisitiza kuvisha hereni mifugo ili kuwatambua kirahisi.





# ‘Msifiche watoto majumbani wapelekeni wapate chanjo’

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, amewataka wazazi pamoja na walezi, kutowaficha watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wawapeleke kwenye maeneo ya kutolea huduma ili wapate chanjo ya Polio.

Dk. Chuachua alitoa kauli hiyo jana wakati akizindua utaoji wa chanjo kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya katika Kata ya Maendeleo mtaa wa Majengo.

Alisema chanjo ya polio haina madhara yoyote kiafya, wazazi wanapaswa kutoa ushirikiano kwa wahudumu wa afya ambao wanazunguka nyumba kwa nyumba kuwapatia matone ya polio watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano.

“Nasisitiza kinamama wote wenye watoto wa umri chini ya miaka mitano mhakikishe wanapata matone ya polio ili kuwakinga na ugonjwa huo hatari, chanjo hiyo haina madhara yoyote kiafya kwani imethibitishwa na mamlaka zote zinazohusika na utoaji wa huduma za afya,” alisema Dk. Chuachua.

Baadhi ya wazazi wanaoshiriki utoaji chanjo waliishukuru serikali kuchukua hatua za mapema katika kukabiliana na ugonjwa huo ambao unadaiwa kuwa hatari kwani hauna tiba zaidi ni kupata chanjo ili kujikinga.

Walisema elimu waliyoipata kutoka kwa watoa huduma iliwasaidia kutambua madhara ya ugonjwa huo na kuwaomba wazazi kuwapeleka watoto wao kupata matone ya polio.

Miongoni mwa watoa huduma ya chanjo ya polio, Aneth Boniface, alisema anaamini zoezi hilo litakuwa rahisi kwa sababu tayari wamewapatia wananchi elimu juu ya umuhimu wa watoto kupata chanjo hiyo.

Alisema kutokana na elimu hiyo, chanjo ya polio itatolewa bila vikwazo na watoto wote wenye sifa ya kupata watafikiwa katika utaratibu uliopangwa.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Dk. Jonathan Lulandala alisema jumla ya watoto 50 walishiriki uzinduzi wa utoaji wa chanjo ya polio jijini humo.

Alisema hatua hiyo inaonyesha namna ambavyo wazazi wamepokea zoezi hilo na wako tayari kuhakikisha watoto wao wanapata matone ya kuwakinga na ugonjwa wa polio.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya imepanga kuwafikia watoto 76,000 wenye umri chini ya miaka mitano ili kuwapatia chanjo hiyo.

Mikoa ya Mbeya na Songwe ambayo inapakana na Malawi, imekwishaanza kupata chanjo itakayodumu kwa siku nne ikiwa ni jitihada za mapambano dhidi ya ugonjwa huo ambao kwa mara ya mwisho nchini uliripotiwa mwaka 1994.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, SACP Ulrich Matei, akiwaonyesha waandishi wa habari ofini kwake jana, fedha taslimu Sh. milioni 26.8 zilizokamatwa kwa mtuhumiwa Mohammed Ally. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Mbaroni tuhuma za wizi wa mil. 26/- za mwajiri

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limemkamata Mohammed Ally (44), mkazi wa Soweto kwa tuhuma za wizi wa Sh. milioni 26.8 anazodaiwa kuiba kutoka kwa mwajiri wake wa Kampuni ya Farmers Center inayojihusisha na uuzaji wa pembejeo za kilimo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, walimnasa mtuhumiwa Februari 28, mwaka huu majira ya saa nane mchana katika maeneo ya Mafiati, jirani na kituo cha mafuta cha Infinity.

Alisema mtuhumiwa Ally akiwa kazini alikabidhiwa Sh. milioni 26.8 na mwajiri wake ili akazipeleke benki akiwa na dereva.

Alifafanua kuwa baada ya dereva kumfikisha benki na kuondoka, mtuhumiwa aliondoka na fedha hizo ambazo alitakiwa kuziweka kama alivyoelekezwa na mwajiri wake na kutokomea kusikojulikana.

Taarifa za tukio hilo ziliripotiwa polisi na ilianza kazi ya upelelezi na kubaini kuwa mtuhumiwa alikwenda Dar es Salaam maeneo ya Ukonga- Mwembe Madafu.

“Machi 16, mwaka huu majira ya jioni, timu ya makachero wa polisi ilianza upelelezi na kufanikiwa kumtia nguvuni mtuhumiwa na katika mahojiano alieleza kuwa fedha hizo alizificha nyumbani kwake jijini Mbeya na askari walifika nyumbani kwake na kufanya upekuzi na kufanikiwa kukuta Sh. milioni 20 zikiwa kwenye mabunda manne,” alieleza Kamanda Matei.

Alisema upelelezi wa shauri hilo unaendelea na utakapokamilika mtuhumiwa atapandishwa kizimbani, aidha Matei alitoa wito kwa jamii kuacha tabia ya tamaa ya kujipatia fedha kwa njia isiyo halali badala yake wajenge tabia ya kufanya kazi kwa bidii na kuwa waaminifu kwa waajiri wao.

# Wizara yaanza kukusanya maoni rasimu sera uwekezaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WIZARA ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kuwatumia watalaam wa masuala ya Uchumi nchini imeanza kukusanya maoni ya wadau juu ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 2022.

Maoni hayo yanalenga kuboresha sekta ya uwekezaji na kukuza uchumi na kupitia utaratibu huo serikali itajua nini mahitaji na maeneo ya kuboresha ili kuvutia wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Akizungumza jana wakati wa kikao cha kupokea maoni ya rasimu hiyo, Mkurugenzi Msaidizi wa Uwekezaji,

Neema Maregeli, alisema ili kutimiza azma ya serikali katika kuimarisha na kuiwezesha sekta binafsi kuwa mhimili wa ukuaji uchumi, wameendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara ili kupunguza umaskini na kuongeza pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Maregeli alisema mwaka 2021, wizara ilikamilisha tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya 1996 ambayo ina malengo mahsusi sita na nane ya kisekta ikiwamo ya kuimarisha uwezo wa ndani wa kukuza uwekezaji na kuhamasisha uzalishaji wa ndani na bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje.

“Rasimu hii inalenga kuondoa urasimu katika utaratibu wa upatikanaji wa vibali vya uwekezaji, sera hii inatoa mwongozo wa uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwamo viwanda, utalii, usafirishaji, kilimo na madini,”alisema Maregeli.

Akizungumzia rasimu hiyo, Mhadhiri Mwandamizi wa Shule Kuu ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Vincent Leyaro, alisema ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau wanaohusika na biashara, uwekezaji pamoja na viwanda unalenga kukaa meza moja na kujadili vikwazo mbalimbali.

Alisema kupitia kikao hicho watakusanya maoni ya mambo gani serikali inapaswa kuyafanya kama vile kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji na kukuza uchumi wa nchi.

Alisema kumekuwa na tatizo kubwa kwa vijana wanaopata nafasi ya kuajiriwa kutokuwa wazalendo pindi wawekezaji wanapoonyesha nia ya kuwekeza wanavutiwa na huduma wanazozipata.

“Miongoni mwa vikwazo vinavyochangia wawekezaji kukimbia katika maeneo yetu ni kutanguliza maslahi binafsi mbele badala ya kuwa na ushawishi wa kuhakikisha anapatiwa eneo na huduma zote muhimu kwa ajili ya kufanya uwekezaji,” alisema Dk. Leyaro.

Alisema hadi sasa jumla ya kanda nne zimefikiwa na timu hiyo ya kukusanya maoni ikiwamo Kanda ya Nyanda za juu Kusini, Kati na Magharibi na kwamba kanda zote zitafikiwa baada ya hapo ripoti itakabidhiwa kwa Waziri wa Viwanda na Uwekezaji tayari kwa kufanyiwa kazi.

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TANESCO

## TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED (TANESCO)

# REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST FOR CONSULTING SERVICES

| | |
|---|---|
| Country | : UNITED REPUBLIC OF TANZANIA |
| Name of Project | : TANZANIA – ZAMBIA TRANSMISSION INTERCONNECTOR PROJECT (TAZA) |
| PRACTICE AREA | : ENERGY AND EXTRACTIVES SPECIFIC PROCUREMENT NOTICE |
| Credit No. | : 6293-TZ |
| Project ID No. | : P163752 |
| Assignment Title | : PROVISION OF CONSULTANCY SERVICES FOR PREPARATION OF ESIA, RAP AND OTHER SAFEGUARD STUDIES FOR UGANDA – TANZANIA TRANSMISSION INTERCONNECTOR PROJECT (UTIP) UNDER TANZANIA – ZAMBIA TRANSMISSION INTERCONNECTOR PROJECT (TAZA) |
| Tender No. | : PA/001/2021-22/HQ/C/13 |
| Reference No. | : TZ-TANESCO-272878-CS-QCBS |
| Issue Date | : March, 2022 |

1. The Government of the United Republic of Tanzania through Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO), has received financing from the World Bank towards the cost of consultancy services for undertaking Environmental and Social Impact Assessment (ESIA), Environmental and Social Management Plan (ESMP), Resettlement Policy Framework (RPF) and other Safeguards studies for Uganda – Tanzania Transmission Interconnector Project (UTIP) through Tanzania – Zambia Transmission Interconnector Project (TAZA) in compliance with Laws of Tanzania and International Standards intends to apply part of the proceeds for consulting services herein.

2. The consulting services ("the Services") include but not limited to the following: -

   (a) Undertake study on Environmental and Social Impact Assessment (ESIA) Study and preparation of ESIA Report;
   (b) Preparation of Stakeholder Engagement Plan (SEP) including grievance redress mechanism (a stand-alone document);
   (c) Preparation of Environmental and Social Management Plan (ESMP) and its sub-plans (e.g., waste management, traffic management, erosion and sediment control plan, health and safety management plan, cultural heritage management, camp management, quarry and borrow pit management and restoration, decommissioning and rehabilitation plan, emergency preparedness and response plan; generic environmental and social specification for construction activities);
   (d) Preparation of Labor Management Procedures (LMP);(annex to ESMP);
   (e) Preparation of SEA/SH Prevention and Response Plan (annex to ESMP);
   (f) Undertake a Biodiversity Management Study and Prepare Biodiversity Management Plan (a stand-alone document); and
   (g) Preparation of Resettlement Policy Framework (RPF) in compliance with the Laws of Tanzania and International Standards.

It is envisaged the scope of the consulting services to be conducted for a total of fifteen (15) months from effectiveness of contract, whereby ESIA studies will be for nine (9) months and RPF and SEP will be for six (6) months. The estimated level of effort is 45 professional staff-months.

3. The detailed Terms of Reference (TOR) for the assignment is available on TANESCO website **(www.tanesco.go.tz).**

4. TANESCO now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the Services. Interested Consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the services referring to the guidance hereunder.

The shortlisting criteria are: -

   (a) Core business and years in business (submit Certificate of Incorporation of the firm and the Company Profile);

   (b) Relevant similar experience which should specifically include: -

# TANGAZO

i. Experience of at least fifteen (15) years in the field of Energy and Power providing consultancy services of similar nature specifically ESIA and Resettlements studies such as RPF, RAP etc. Please, submit at least one Project Completion Certificate detailing the scope performed in the last fifteen (15) years. The Certificate must include the contact details of the Client, Issue date and the Form of Contract showing that such contract(s) was/were performed in the last 15 years.

ii. Experience in consultancy services related to Transmission line projects with voltage level of 220kV and above having executed five (5) or more similar assignments within the last ten (10) years. The Applicant shall prepare a Table Summary with the following information for completed power transmission projects with voltage level of 220kV and above executed within the last ten (10) years: (i) Project Name, (ii) Contract Number, (iii) Contract Value, (iv) Contract Signing Date, (v) Original Completion Date, (vi) Actual Completion Date and reasons if the completion date was delayed, (vii) Voltage Level of the Project, (viii) Route Length, (ix) Country where the project is located, (x) Project Location, (xi) Employer's Name, (xii) Employer's Address, (xiii) Project Financier, and (xiv) Brief Description of the Scope Performed in not more than two pages. Please refer **Section 8: Consultant Experience and Study Team of the ToR** for more guidance and clarity. If in the submitted experience the Firm participated as partnership/association/consortium in the Form of JV or Lead Firm or Sub-consultant, please state the role performed (Prime or JV or Sub-Consultant) and the details of scope executed.

iii. Demonstration of experience of working in similar conditions specifically in developing countries.

(c) Demonstration of technical and managerial capability of the firm (provide only the entire Structure of the Organization/Firm, Organization Structure specific for this assignment, general qualifications, relevant number of key-staff meeting the requirements of this assignment, and list of completed projects accompanied with completion certificates and other relevant details in the form advise under Paragraph 4(b)(ii) hereinabove). Please, do not provide the Curriculum Vitae (CV) of key staff at this shortlisting stage, **as the CV of Key Experts will not be evaluated at shortlisting stage, only allocate the required number of Key-Staff as preset in the ToR.**

5. The attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, 3.17, 3.18 of the World Bank's Procurement Regulations November 2020 (Fourth Edition), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest and unfair competitive advantage. Firm intending to submit an expression of interest should not have a conflict of interest and unfair competitive advantage as per Bank's Procurement Regulations.

6. Consultants may associate with other firms to enhance their qualifications, but should indicate clearly whether the association is in the form of a joint venture and/or a sub-consultancy. In the case of a joint venture, all the partners in the joint venture shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected. Therefore, each member of JV should independently meet the requirements of the evaluation criteria. The maximum number of members in a JV is two (2). The firm/s must not appear in more than one application as such shall lead to disqualification of all applications right from this shortlisting stage except for Sub-Consultant(s). The Technical and Managerial Capability of the Sub-Consultant shall not be evaluated to enhance the qualification of the Applicant.

7. A Consultant will be selected in accordance with the Quality and Cost Based Selection (QCBS) method set out in the World Bank's Procurement Regulations.

8. Further information can be obtained at the address below during office hours 0800 **Hours up to 1700 Hours East African Time on Monday to Friday** inclusive except weekends and public holidays:

***Secretary TANESCO Tender Board***

**TANESCO Office,**
**Third Floor, Room No. A 305,**
**Umeme Park Building,**
**Morogoro Road, Ubungo Area**
**P.O. Box 9024,**
**Dar es Salaam.**
**TANZANIA.**

**Email:** *sec.tenderboard@tanesco.co.tz;*
**Copy:** *pmuprojects@tanesco.co.tz*

9. For clarification purposes and, the Employer's address is: -

**Secretary TANESCO Tender Board,**

**P.O Box 9024,**
**Dar es Salaam – Tanzania**
**Attn.: Ms. Rehema O. Shabani,**

**Address:** Morogoro Road, Ubungo Area,
Umeme Park Building, 3rd Floor,
Room No. A305.
City: Dar Es Salaam
Country: TANZANIA
Telephone: +255 222 210 231/232
Email:
*sec.tenderboard@tanesco.co.tz*
*Cc: pmuprojects@tanesco.co.tz*

**Must copy the following:**
Mr. Peter E. Kigadye,
*peter.kigadye@tanesco.co.tz*
Mr. Elias J. Makunga,
*elias.makunga@tanesco.co.tz*
Mr. Timothy Mgaya,
*timoth.mgaya@tanesco.co.tz*
Mr. David Kapongo,
*david.kapongo@tanesco.co.tz*
Mr. Raymond Mbaga,
*raymond.mbaga@tanesco.co.tz*

The clarifications response and/ or addendums shall be posted on TANESCO Website https://www.tanesco.co.tz/index.php/procurement/current-tenders for applicants to comply.

10. Expressions of interest in English Language must be submitted in a clearly marked envelopes and delivered to the following address (in personal or by e-mail through address: taza.consulting@tanesco.co.tz) on or before **Wednesday 20th April, 2022 at 10:30 Hours East African Time:** In addition to the original hard copy, the number of copies to be submitted with the Application is: Two (2) hard copies and three (3) soft copies in separate USB Flash drives in read only format. Any discrepancies between the original and the copy/ or copies, the original document shall prevail. Failure to comply with the requested number of submissions, the Client may reject the Application Submission. In the Application Submission Letter, please, clearly state the Name of the Consulting Firm, the Physical Address, Postal Address, Valid E-mail Address, Website, and Telephone Numbers. In case of association/ partnership/ consortium please, state clearly if is a Joint Venture (JV) partnership/association/consortium or is a Lead Firm with other partner/associate/consortium member(s) as Sub-consultant(s). For any partnership/association/consortium each member must provide full details of its addresses as directed hereinabove.

**Secretary TANESCO Tender Board**

**TANESCO Office,**
**Ground Floor, Room No. G 04,**
**Umeme Park Building,**
**Morogoro Road, Ubungo Area**
**P.O. Box 9024,**
**Dar es Salaam.**
**Tanzania.**
**Email: (taza.consulting@tanesco.co.tz)**

**MANAGING DIRECTOR**
**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LTD**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

FORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 157 OF 2022**
**In The Matter Of the Estate of the Late**
**EDWARD GERSON KIWIA**
**And**
**In the Matter Of Application for Letters of Administration by PRIME EDWARD KIWIA**

## GENERAL CITATION

**[RULE 75]**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate [or letters of administration] is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12 day of 04 /2022

Dated at DAR ES SALAAM this 21 day of 03 /2022

Registrar/Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ANTIDIUS MIHANGAIKO ALUMERY** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC247 CEH. CHASSIS NAMBA LBRSPJB53K9000412.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAG/BIH/RB/112045/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMSON PETER MOYO** wa kampuni ya Shilo Construction ya Songea, Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 866 ALLY** aina ya Toyota Hilux Surf rangi ya blue . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa imeripotiwa polisi **MKB/ TR /RB/55/2022.**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**
**MISC LAND CASE APPLICATION 138/2021**
**(Originating arise from land Application no. 103 of 2019 at Muleba DLHT)**
**CHARLES BUCHWA ...........APPLICANT**
**VERSUS**
**ALLY ABDU MABARAZA .........1ST RESPONDENT**
**JONAS CHARLES ..................2ND RESPONDENT**
**TO, JONAS CHARLES OF KASHAI WARD BUKOBA MUNICIPALITY**

### RE: NOTICE FOR DATE OF HEARING

Whereas the above mentioned Appellants has lodged a case registered as Misc Land case application no. 138/2021 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for hearing on 12th day of April, 2022 at 08:30 am before Hone Mwipopo J. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 15th day of March, 2022.

JANETH MASESA
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA BUKOBA MJINI, MKOA WA KAGERA**
**SHAURI LA MADAI/NDOA NA. 9/2022**
**Jina la Mdai ..................PROSCOVIA PETER**
**Jina la Mdaiwa ................ISACK BAMANYISA**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

Kwa: ISACK BAMANYISA

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao ya Talaka, Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 04 Mwezi 04 Mwaka 2022 saa 2:00 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo.

Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 21 Mwezi 03 Mwaka 2022.

..............................................
**HAKIMU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**
**SHAURI LA TALAKA NA 7/2020**

**GEORGE JOSEPH MASAMBU..................MDAI**
**VS**
**TUPOKIGWE ELIAS MWAKAJUMBA.................MDAIWA**

### MAOMBI YA TALAKA

Unatakiwa kufika mahakamani tarehe 01/04/2022 saa 2:30 asubuhi kwa ajili ya shauri la talaka usipofika shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 24/03/2022.

..............................................................
**HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO**
**IRINGA MJINI**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA MOROGORO
LILILOPO MOROGORO
MAOMBI MADOGO NAMBA 31 YA 2022
GERALD MISINZO...........................MUOMBAJI
DHIDI YA
JULIANA JERRY
ARMSTRONG.....................MJIBU MAOMBI

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**JULIANA JERRY ARMSTRONG** popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 25/4/2022 mbele ya Mwenyekiti E.Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI Baraza leo tarehe 23 Mwezi Machi, 2022.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya CHAMWINO
Kituo cha MOROGORO Mkoa Wa MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi Na......8..2021
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU RAMADHANI ABDALLAH MHINDA WA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA SHABAN RAMADHAN

### TANGAZO

(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 13 Mwezi 04 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 15 Mwezi 03 Mwaka 2021

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**
**MISC LAND CASE APPLICATION 138/2021**
**(Originating arise from land Application no. 103 of 2019 at Muleba DLHT)**
**CHARLES BUCHWA ...........APPLICANT**
**VERSUS**
**ALLY ABDU MABARAZA .........1ST RESPONDENT**
**JONAS CHARLES ..................2ND RESPONDENT**
**TO, JONAS CHARLES OF KASHAI WARD BUKOBA MUNICIPALITY**

### RE: NOTICE FOR DATE OF HEARING

Whereas the above mentioned Appellants has lodged a case registered as Misc Land case application no. 138/2021 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for hearing on 12th day of April, 2022 at 08:30 am before Hone Mwipopo J. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 15th day of March, 2022.

JANETH MASESA
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT DODOMA**
**APPELLATE JURISDICTION**
**CRIMINAL REVISION NO. 01 OF 2022**
**(FROM ORIGINAL CRIMINAL CASE NO.18 OF 2018**
**IN THE RM'S COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**DPP.................................APPELLANT/APPLICANT**
(Original accused /Prosecutor)
**VERSUS**
**THADEI BONIFACE KAYOMBO & 2**
**OTHERS................................... RESPONDENT**
(Original accused /Prosecutor)

**TO THADEI BONIFACE KAYOMBO**

**TAKE NOTICE** that the 05 day of **04,2022 at 9:00 O'clock** in the forenoon has been fixed for the Mention/Hearing/Judgement/Ruling of the appeal against conviction and sentence filed by the Applicant in the above case.

Given under my hand and the seal of the Court this **17 day of 03,2022**

DEPUTY REGISTRAR
DODOMA

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT DODOMA**
**APPELLATE JURISDICTION**
**CRIMINAL REVISION NO. 01 OF 2022**
**(FROM ORIGINAL CRIMINAL CASE NO.18 OF 2018**
**IN THE RM'S COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**DPP.................................APPELLANT/APPLICANT**
(Original accused /Prosecutor)
**VERSUS**
**THADEI BONIFACE KAYOMBO & 2**
**OTHERS................................... RESPONDENT**
(Original accused /Prosecutor)

### TO ADELHAD MGENI

**TAKE NOTICE** that the 05 day of **04,2022 at 9:00 O'clock** in the forenoon has been fixed for the Mention/Hearing/Judgement/Ruling of the appeal against conviction and sentence filed by the Applicant in the above case.

Given under my hand and the seal of the Court this **17 day of 03,2022**

DEPUTY REGISTRAR
DODOMA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya NJOMBE
Kituo cha Njombe Mjini
Mkoa Wa Njombe
Usimamizi wa Mirathi Na...21...2022
Katika shauri la mirathi ya
ROMWALD FRANCIS KINYERO MAREHEMU
WA KAMBARAGE
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA THOBIAS JAFARI MOHAMED

### TANGAZO KWA UMMA

(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 03 Mwezi 04 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. MAPINGAMIZI YOYOTE KUHUSU MAOMBI HAYA YAWE YAMEANDIKISHWA KABLA AU MPAKA TAREHE TAJWA HAPO JUU

Imetolewa leo tarehe ......10..... Mwezi...03....mwaka .....2022

HAKIMU MKAZI

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO 40 OF 2022

In the Matter of the Estate of the Late
ESTHER DANIEL MAGAFU

By 1. DEUSDEDIT MAGAFU BILINGI
2. ........................................................

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 06th day of April..... 2022

Dated at MOROGORO this 23rd day of March.........2022

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HILLARY MASHOKO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 208 DCS – TOYOTA CARINA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/118348/202**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# RAGE AIPA YANGA UBINGWA

**Na Adam Fungamwango**

KIONGOZI wa zamani wa Simba, na Chama cha Soka Nchini (FAT), Ismail Aden Rage amesema kuwa Yanga ina nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa msimu huu na wanastahili kutokana na kuwa na kikosi kizuri.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Rage ambaye alikuwa mwenyekiti wa zamani wa Simba, alisema ukweli lazima usemwe kuwa msimu huu Yanga wamefanya usajili mzuri na wana wachezaji wenye viwango vya juu, hivyo wanastahili kuwa mabingwa.

"Japo mimi ni Simba, na natamani sana Yanga wapoteze mechi ili timu yangu iwe bingwa, lakini kila ukiangalia watani zetu msimu huu wako vizuri, wamesajili vizuri, wana wachezaji wazuri, kwa hiyo ni ngumu sana kupoteza mechi nyingi ili sisi tuwe mabingwa ingawa napenda litokee hilo," alisema Rage.

Kiongozi huyo wa zamani wa FAT, pia alimsifu Straika wa Yanga Fiston Mayele akisema ana sifa zote za kuwa mshambuliaji mzuri, kwani anajua kufunga na pia ana nguvu, akimfananisha na Ronaldo De Lima.

"Yule unaweza kumfananisha na Ronaldo, anajua kipa amekaa wapi na mimi nipige wapi, ana nguvu, ana spidi, kusema kweli ni straika mzuri, ila kiboko yake ni yule beki wa Simba Enock Inonga, Mkongomani mwenzie ambaye siku ile ya mechi ya watani hakufurukuta mpaka akasindikizwa kutoka nje," alisema Rage huku pia akiweka utani wa klabu hizo mbili kama kawaida.

Yanga inaongoza Ligi Kuu mpaka sasa ikiwa na pointi 48, pointi 11 nyuma ya timu inayomfukuza Simba, yenye 37, ikiwa imefunga mabao 31, kumi yakiwa yamefungwa na straika wao hatari waliyemsajili msimu huu kutoka AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Mayele.



Mchezaji wa timu ya Mbande Veteran, Yahaya Amanzi (kushoto), akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wenzake wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Chamazi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Muumin, Hafsa Kazinja waja na 'Tusiachane'*

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI mkongwe wa muziki wa dansi, Mwinjuma Muumin, ameibuka na wimbo mpya ambao ameupa jina la 'Tusiachane' wa mtindo wa zouk akiwa amemshirikisha mwimbaji Hafsa Kazinja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Muumin ambaye pia ni Mkurugenzi wa Special Bend, alisema wimbo huo ni wake binafsi siyo wa bendi hiyo na kwamba amefanya hivyo ili kupata vionjo tofauti.

"Kama unamfuatilia Christian Bella utagundua kuwa ana nyimbo zake binafsi, lakini pia zipo za bendi, ndivyo hata mimi ninafanya ili kupata vionjo tofauti, hasa kutokana na ukweli kwamba Kazinja ni miongoni mwa waimbaji wazuri wa zouk hapa nchini,"alisema Muumin.

Muumin alisema, kwa sasa wapo studio wakiendelea kurekodi wimbo huo ili baadaye ausambaze katika vituo mbalimbali vya redio na kisha kuandaa video na kuiweka pia kwenye mitandao ya kijamii.

Alisema, muziki wa dansi kwa sasa unakumbana na changamoto nyingi, na kwamba njia ya kukabiliana nazo ni kubuni mbinu mbalimbali za kuhakikisha wanaendelea kuendesha maisha kwa kutegemea muziki huo.

"Kwa hiyo njia mojawapo ni kushirikisha wanamuziki wa dansi, zouk, bongofleva ili kuhakikisha tunawapata mashabiki wote kwa pamoja wakati huu ambao dansi liko kipindi cha mpito," alisema.

Muumin aliyewahi kutamba na nyimbo mbalimbali zikiwamo za 'Tunda na Mgumba' zilizompa umaarufu mkubwa, alisema ana uhakika muziki huo ukipewa nafasi ya kutosha katika vyombo vya habari utarudi kwenye chati.

Alisema, yeye hawezi kukata tamaa kutokana na changamoto ambazo muziki huo unapitia, badala yake anaendelea kukomaa hadi kieleweke na kwamba hakubaliani na kauli kuwa dansi zimepitwa na wakati. "Hivyo niwaambie wanamuziki wenzangu kuwa tusikate tamaa, tuendelee kupambana ili kuhakikisha tunarudisha muziki huu kwenye chati hasa kwa kupendana wenyewe kwa wenyewe badala kukatishana tamaa," alisema.

## Kaseja hajafikiria kustaafu soka

**Na Adam Fungamwango**

KAMA kuna mashabiki walitegemea kuwa golikipa mkongwe nchini Juma Kaseja yuko kwenye miaka ya mwisho kustaafu soka wafute mawazo hayo, kwani mwenyewe ameweka wazi kuwa ataendelea kucheza soka na hatarajii kustaafu miaka ya hivi karibuni.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Kaseja amesema kuwa hawezi kuacha soka kwa sababu hana kazi nyingine ya kufanya, na hadhani kama ana urithi wa kuwaachia watoto wake, zaidi ya yeye kusakata kabumbu ili awatunze na kuwasomesha.

"Unajua kuna watu wanahesabu tu miaka mingi ambayo mimi nimecheza soka, lakini hawawezi kuangalia wakati naanza kucheza soka nilikuwaje. Mimi nimeingia kwenye soka bado mdogo sana, lakini watu wanaangalia tu miaka. Kama kuna mtu anadhani nitaacha soka hivi karibuni asahau. Bado nipo nipo sana kwenye soka, siwezi kuacha mpira kwa sababu sina kazi nyingine ya kufanya, sidhani kama nina urithi wa kuwaachia watoto wangu, lakini kikubwa zaidi ni kwamba uwezo wa kucheza ninao, kudaka ni kazi yangu na kuokoa ni kazi yangu," alisema Kaseja.

Kipa huyo ambaye timu yake ya KMC ilichapwa mabao 2-0 dhidi ya Yanga, ana zaidi ya miaka 20 kwenye soka kwa sasa.

Alishawahi kuzidakia timu za Mkunguni na IPP za Dar es Salaam mwishoni mwa miaka ya 1990, kabla ya kutimkia Moro United, na kwa muda mfupi alijiunga na Mtibwa Sugar kabla ya kujiunga na Simba mwanzoni mwa miaka ya 2000, na alipata jina kubwa 2003, akiwa langoni kwenye kikosi cha Simba kilichowatikisa Mabingwa Watetezi wa Afrika wakati huo, Zamalek ya Misri kwa mikwaju ya penalti na kutinga hatua ya makundi. Alizidakia pia timu za Yanga, Mbeya City na Kagera Sugar.

## Makata aahidi kuibakisha Mbeya Kwanza

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu mpya wa Mbeya Kwanza, Mbwana Makata amefunguka kwa mara ya kwanza baada ya kukabidhiwa mikoba ya kukinoa kikosi, akisema kuwa kazi yake kubwa ni kuibakisha timu hiyo Ligi Kuu.

Makata amesema kuwa mara baada ya kupewa kazi hiyo amekutana na wachezaji wa timu hiyo na kuwaweka vizuri kisaikolojia, huku mikakati yake ikiwa ni kuhakikisha timu hiyo haishuki daraja.

"Nimeongea na wachezaji wangu, tumeongea mengi na nimewaweka sawa kisaikolojia, kwa hiyo kazi yangu kubwa ni kuhakikisha timu haishuki daraja, badala yake inabaki Ligi Kuu, kitu ambacho kinawezekana kabisa," alisema kocha huyo.

Alisema kuwa ili timu isalie ni lazima aifanye ishinde mechi na isifungwe, hivyo kazi kubwa ni kuhakikisha anaimarisha idara mbili, ya ulinzi na ushambuliaji.

"Nitaimarisha kwanza idara ya ulinzi ili isiruhusu mabao, lakini pia kuinoa safu ya ushambuliaji ili tufunge mabao yatakayotufanya tubaki Ligi Kuu, baada ya hapo sasa tunaangalia na idara nyingine ambazo nitakuwa nikizirekebisha taratibu," alisema Makata.

Meneja wa klabu hiyo Davis Naftari amesema ujio wa kocha huyo unaweza kuwa mkombozi kwa timu hiyo kwa sababu morali ya wachezaji ilishuka.

Makata amejiunga na Mbeya Kwanza, baada ya kutimuliwa Dodoma Jiji, mwishoni mwa Februari, baada ya timu hiyo kutofanya vema kwenye mechi za Ligi Kuu.

Kwa sasa Mbeya Kwanza ambayo imehamishia mechi zake za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Majimaji Songea, iko kwenye nafasi ya 15, ikiwa na pointi 14 kwa michezo 18 iliyocheza.

## ZISIKUPITE

**KANE AKATAA**
MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, amekataa kuweka wazi mustakabali wake baada ya kuulizwa kuhusu mustakabali wake akiwa kwenye majukumu ya timu ya taifa ya England. (***Mirror***)

**RICE ANAITAKA CHELSEA**
KIUNGO wa timu ya taifa ya England, Declan Rice angependelea kuhamia Chelsea badala ya Manchester United ikiwa ataondoka West Ham, ambao wameweka bei ya pauni milioni 150 ili kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. (***Evening Standard***)

**NEYMAR HATAKIWI**
KLABU ya Newcastle United haitamnunua mshambuliaji wa Paris St-Germain, Neymar mwenye umri wa miaka 30, na wanajiandaa kuwa na bajeti ya uhamisho ya msimu wa joto ambayo itakuwa chini ya pauni milioni 90 ukilinganisha na ile walitumia Januari. (***Telegraph***)

**ALMIRON KUONDOKA**
MPANGO wa Newcastle ni kumuuza kiungo wa kati wa Paraguay, Miguel Almiron msimu wa joto na watamruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kuondoka kwa pauni milioni 15. (***Football Insider***)

**NUNEZ ATAKIWA ARSENAL**
KLABU ya Arsenal inamfuatilia mshambuliaji wa Benfica, Darwin Nunez na wamefanya mazungumzo na wakala wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 22. (***Express***)

**BOTMAN AGOMBEWA**
KLABU ya West Ham inamnyatia mlinzi wa Uholanzi, Sven Botman lakini watakabiliwa na ushindani kutoka kwa Newcastle United na AC Milan ikiwa wataamua kumsajili kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22 kutoka Lille. (***Evening Standard***)

**KESSIE AWANIWA**
KLABU za Tottenham Hotspur, PSG na Real Madrid zinamtaka kiungo wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 atajiunga na Barcelona wakati mkataba wake utakapomalizika AC Milan msimu wa joto. (***El Nacional***)

**CESAR APUUZA**
MLINZI wa Hispania, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32 amepuuza madai kuhusu mustakabali wake katika klabu ya Chelsea huku kukiwa na tetesi kwamba huenda akajiunga na Barcelona msimu huu wa joto. (***Goal***)

**SALIBA NA HATIMA**
MLINZI wa Ufaransa, William Saliba, ambaye yuko Marseille kwa mkopo kutoka Arsenal, amesema hatima yake ya baadaye itategemea mazungumzo na Washikabunduki hao. Mkataba wa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 20 unamalizika mwaka 2024. (***RMC Sport, via Goal***)

**ARAUJO HAONGEZEWI**
KLABU ya Barcelona haina nia ya kuongeza ofa yao kwa beki wa Uruguay, Ronald Araujo, huku mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 nao ukikamilika 2023. (***Catalunya Radio***)

**ABRAMOVICH KUINUNUA GOZTEPE**
MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich ameripotiwa kuanzisha mazungumzo ya kununua klabu ya Goztepe inayoshiriki Ligi Kuu ya Uturuki. (***Fanatik, via Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ORIGI KUTIMKA LIVERPOOL

## Afanya mazungumzo na AC Milan, Inter na anaweza kuondoka kwa uhamisho huru...

**LIVERPOOL,** ENGLAND

DIVOCK Origi ameiambia Liverpool kuwa anafikiri ni wakati wa kuondoka katika klabu hiyo na yuko kwenye mazungumzo na AC Milan na Inter Milan kuhusu uhamisho wa bure, kwa mujibu wa mtandao wa 90minutes.

Origi ni mchezaji wa kikosi cha thamani chini ya Jurgen Klopp lakini amepunguzwa kwa dakika 71 tu za kucheza Ligi Kuu ya England katika mechi tano akitokea benchi msimu huu, huku usajili wa Januari wa Luis Diaz ukimfanya asipewe nafasi.

Huku mkataba wake ukikamilika mwishoni mwa msimu huu, vyanzo vimethibitisha kwamba, Liverpool walikuwa tayari kumpa Origi mkataba mpya, lakini Mbelgiji huyo amedokeza kuwa yuko tayari kusonga mbele na kutafuta nafasi zaidi za kikosi cha kwanza.

**Origi hajaanza mara kwa mara katika klabu ya Liverpool tangu msimu wa 2016/17, akianza mechi saba za ligi msimu wa 2019/20 na mbili pekee mwaka jana.**

Akiwa na nafasi katika kikosi cha Ubelgiji kwenye Kombe la Dunia la 2022, Origi anafahamu vyema kwamba anahitaji kucheza mara kwa mara.

AC Milan wanafahamika kuwa mstari wa mbele katika msimamo wake, lakini wapinzani na majirani zao Inter pia wameonesha nia ya kumuwania Origi, huku timu za Hispania na Ujerumani pia zikiwasiliana.

Origi pia amezivutia timu nyingi za Ligi Kuu England, lakini inaonekana kama atachagua kutafuta changamoto mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa kiasi fulani ni shujaa wa Liverpool baada ya kufunga mabao kadhaa muhimu wakati alipokuwa klabuni hapo, mara nyingi akitokea benchi.

Origi alifunga bao la nne na la kuamua katika ushindi wa kushangaza dhidi ya Barcelona kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 1,065

MECHI KALI
FRANCE
VERSUS
IVORY COAST
1 | 1.38
X | 4.65
2 | 8.49

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SILVA KUCHEZA HADI MIAKA 40




**LONDON,** England

MCHEZAJI Thiago Silva amefichua kuwa anatamani kumuiga gwiji wa AC Milan, Paolo Maldini kwa kuendelea kucheza katika kiwango cha juu hadi kufikia umri wa miaka 40.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 alijiunga na Chelsea mwaka wa 2020 kwa uhamisho wa bure kutoka Paris Saint-Germain, licha ya sifa yake ya kuwa mmoja wa beki bora wa kati wa kizazi chake, bado hajafikia matarajio pale Stamford Bridge.

Thiago tayari amesaini mkataba wa mwaka mmoja zaidi na The Blues hao ambao utamuweka katika klabu hiyo hadi miezi michache kabla ya kutimiza miaka 39 mwaka 2023, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil amefichua kuwa hana mpango wa kuacha kucheza wakati huo - akitarajia kumuiga gwiji wa moja ya vilabu vyake vya zamani.

"Natumai ninaweza kufanya kile ambacho Maldini alifanya kule Milan, akicheza hadi alipokuwa na umri wa miaka 40 au 41," aliambia tovuti rasmi ya Chelsea.

"Huo ni mpango wangu wa siku za usoni na nimejitayarisha kwa hilo."

Hata hivyo, wakati Thiago akipanga kuendelea kucheza kwa miaka kadhaa zaidi, pia alikiri kwamba mwili wake unachukua muda mrefu kupona akipata majeraha.



## Chelsea yaruhusiwa kuuza tiketi

**LONDON,** England

CHELSEA itaruhusiwa kuuza tiketi za michezo ya ugenini, mechi za mataji zinazohusisha timu ya wanawake baada ya serikali ya Uingereza kufanya mabadiliko kwenye leseni maalum ya klabu hiyo.

Klabu hiyo haikuweza kuuza tiketi tangu mmiliki Roman Abramovich alipowekewa vikwazo na serikali kama sehemu ya majibu yake kwa uvamizi wa Russia dhidi ya Ukraine.

Chini ya leseni iliyobadilishwa, mapato yatokanayo na mauzo ya tiketi yataenda moja kwa moja kwenye Ligi Kuu.

Hatua hiyo ina maana kwamba Chelsea wataweza kuuza tiketi za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid Aprili 6 na nusu fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Wembley Aprili 16 dhidi ya Crystal Palace.

Mashabiki wa ugenini wanaweza kununua tiketi za michezo ya Ligi Kuu pale Stamford Bridge, na mapato yataenda kwa Ligi Kuu.

Chelsea wameomba kwamba fedha zozote zinazotokana na mauzo ya tiketi, ambazo klabu ingekuwa nazo kwa kawaida, zitolewe kwa waadhiriwa wa vita nchini Ukraine.

5,872,000

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/03/2022 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Cambridge Utd | 2.29 | 3.29 | 2.95 |
| 02. 26/03/2022 | 18:00 | Airdrieonians vs Cove Rangers | 2.73 | 3.27 | 2.42 |
| 03. 26/03/2022 | 18:00 | Elgin City vs Edinburgh City | 2.42 | 3.20 | 2.67 |
| 04. 26/03/2022 | 18:00 | Peterhead vs Falkirk FC | 2.78 | 3.32 | 2.35 |
| 05. 26/03/2022 | 18:00 | Leyton Orient vs Barrow | 2.24 | 3.29 | 3.04 |
| 06. 26/03/2022 | 18:00 | Carlisle vs Bristol Rovers | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 07. 26/03/2022 | 18:00 | Colchester vs Tranmere | 2.40 | 3.28 | 2.79 |
| 08. 26/03/2022 | 18:00 | Bradford City vs Newport | 2.56 | 3.20 | 2.66 |
| 09. 26/03/2022 | 18:30 | Den Bosch vs VVV Venlo | 2.36 | 3.72 | 2.55 |
| 10. 26/03/2022 | 19:00 | Finland vs Iceland | 2.28 | 3.15 | 3.30 |
| 11. 27/03/2022 | 15:00 | Mirandes vs Ponferradina | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 12. 27/03/2022 | 17:00 | Burgos vs Tenerife | 3.05 | 3.00 | 2.39 |
| 13. 27/03/2022 | 19:15 | Malaga vs Huesca | 2.49 | 3.08 | 2.83 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 25/03/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4127 | Uganda vs Tajikistan | 2.01 | 3.33 | 3.83 |
| 15:00 | 2593 | Latvia vs Kuwait | 2.25 | 3.32 | 3.17 |
| 15:00 | 5140 | Southampton U23 vs Wolverhampton U23 | 2.72 | 3.54 | 2.22 |
| 16:30 | 1270 | Millwall U23 vs Colchester U23 | 2.05 | 3.70 | 2.92 |
| 17:00 | 3567 | Bosnia and Herzegovina U21 vs Luxembourg U21 | 1.17 | 6.04 | 12.66 |
| 18:00 | 3345 | Azerbaijan U21 vs Estonia U21 | 1.53 | 3.84 | 5.44 |
| 18:00 | 3742 | Slovakia U21 vs Northern Ireland U21 | 1.42 | 4.18 | 6.41 |
| 19:00 | 5486 | Hradec Kralove vs Slovacko | 3.01 | 3.20 | 2.19 |
| 20:00 | 4144 | FC KoÅiice vs MSK Namestovo | 1.09 | 8.18 | 16.55 |
| 20:00 | 4250 | GKS Wikielec vs MKS Kutno | 2.08 | 3.21 | 3.25 |
| 20:00 | 4378 | Norway vs Slovakia | 1.76 | 3.44 | 4.96 |
| 20:00 | 4454 | Kosovo U21 vs Slovenia U21 | 4.17 | 3.49 | 1.74 |
| 20:00 | 5631 | Croatia U21 vs Austria U21 | 1.85 | 3.60 | 3.55 |
| 20:00 | 5863 | Opava vs Dukla Prague | 2.09 | 3.31 | 3.12 |
| 20:15 | 1425 | Germany U21 vs Latvia U21 | 1.01 | 11.67 | 38.91 |
| 20:30 | 2178 | Montenegro U21 vs Italy U21 | 6.05 | 3.90 | 1.47 |
| 20:45 | 5961 | Bulgaria U21 vs Netherlands U21 | 6.61 | 4.47 | 1.38 |
| 21:00 | 1330 | Sete 34 FC vs Concarneau | 4.25 | 3.16 | 1.88 |
| 21:00 | 1412 | Cholet vs Annecy FC | 3.07 | 3.12 | 2.28 |
| 21:00 | 2556 | Switzerland U21 vs Wales U21 | 1.33 | 4.76 | 7.19 |
| 21:00 | 2853 | Malta vs Azerbaijan | 3.38 | 3.23 | 2.20 |
| 21:00 | 3149 | Avranches vs Orleans | 2.87 | 3.02 | 2.47 |
| 21:00 | 3665 | Chateauroux vs Boulogne | 1.61 | 3.46 | 5.73 |
| 21:00 | 4082 | Le Mans vs Red Star | 2.96 | 2.96 | 2.45 |
| 21:00 | 4490 | Skive IK vs Kolding IF | 2.27 | 3.16 | 2.92 |
| 21:00 | 4555 | B 93 Copenhagen vs AB Gladsaxe | 1.94 | 3.40 | 3.45 |
| 21:00 | 4616 | Albania U21 vs Czech Republic U21 | 6.82 | 3.99 | 1.42 |
| 21:00 | 4685 | Saint Brieuc vs Sedan | 2.14 | 2.91 | 3.65 |
| 21:00 | 4774 | Bastia Borgo vs Villefranche Sur Saone | 3.58 | 3.09 | 2.07 |
| 21:00 | 5568 | Creteil vs Chambly | 2.47 | 3.02 | 2.87 |
| 21:15 | 1580 | Romania vs Greece | 2.64 | 2.99 | 2.89 |
| 22:00 | 2191 | Poland U20 vs England U20 | 4.20 | 3.40 | 1.85 |
| 22:00 | 4930 | Spain U21 vs Lithuania U21 | 1.01 | 12.65 | 43.77 |
| 22:00 | 5014 | NK Nafta vs NK Bilje | 1.38 | 5.00 | 6.80 |
| 22:05 | 1720 | Scotland U21 vs Turkey U21 | 2.12 | 3.26 | 3.11 |
| 22:15 | 4765 | Luxembourg vs Northern Ireland | 3.17 | 3.17 | 2.33 |
| 22:30 | 3420 | LKS Lodz Pss vs Miedz Legnica | 3.17 | 3.27 | 2.09 |
| 22:45 | 3440 | Bray Wanderers vs Wexford Youths | 2.02 | 3.45 | 3.16 |
| 22:45 | 3959 | Treaty United vs Waterford Utd | 4.29 | 3.65 | 1.69 |
| 22:45 | 4081 | Cork City vs Athlone Town | 1.22 | 5.65 | 9.75 |
| 22:45 | 4887 | England U21 vs Andorra U21 | 1.01 | 14.62 | 68.22 |
| 22:45 | 5482 | Bosnia and Herzegovina vs Georgia | 1.83 | 3.48 | 4.44 |
| 22:45 | 5540 | Longford Town vs Galway United | 3.17 | 3.31 | 2.07 |
| 22:45 | 5909 | Larne vs Ballymena Utd | 1.39 | 4.59 | 6.24 |
| 23:00 | 1529 | FC Eindhoven vs De Graafschap | 2.47 | 3.26 | 2.67 |
| 23:00 | 3298 | Aberystwyth Town vs Barry Town FC | 2.25 | 3.40 | 2.77 |
| 23:00 | 3318 | Zaragoza vs Amorebieta | 1.88 | 3.07 | 4.46 |
| 23:00 | 5733 | Dordrecht vs ADO Den Haag | 3.95 | 3.95 | 1.73 |
| 23:15 | 3554 | Portugal U21 vs Iceland U21 | 1.13 | 7.02 | 13.65 |
| 23:15 | 5974 | France vs Ivory Coast | 1.38 | 4.65 | 8.49 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WASHINDI SPORTPESA BET BONANZA WATANGAZWA

**Na Dennis Fussi**

WASHINDI watatu Masoud Abdallah, Omari Saidi na Charles Joseph jana wameibuka washindi wa vitita vya shilingi 1,000,000 kila mmoja katika droo ya pili ya wiki ya Bet Bonanza ya SportPesa.

Droo hiyo ni sehemu ya promosheni ya Bet Bonanza ya Sportpesa, na pia ni mwendelezo wa zawadi ambazo zinatolewa katika kipindi hiki cha ligi mbalimbali zinazochezwa kwa ushirikiano na kampuni za simu Vodacom, Airtel na Halotel.

Akizungumza baada ya droo iliyochezeshwa makao makuu ya SportPesa Oysterbay, Dar es Salaam, Meneja Uhusiano wa kampuni ya SportPesa, Sabrina Msuya amesema droo ya pili katika wiki ya pili ya Bet Bonanza wateja wa Vodacom, Airtel na Halotel wamejishindia vitita vya shilingi milioni moja moja kwa kila mmoja.

"Kama mnavyofahamu leo (jana) imechezeshwa droo yetu ya pili ya wiki ya Bet Bonanza ambapo wateja watatu kutoka Mkuranga - Pwani, Manyoni Singida na Dumila, wameshinda shilingi milioni moja moja, baada ya kubashiri na kuibuka washindi wa Bet Bonanza ya Sportpesa," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Vodacom, Meneja Mauzo wa M-Pesa, kutoka kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom, Kelvin Nyanda alisema wachezaji wa SportPesa ambao wanatumia laini za simu za Vodacom hawana budi kuiga mfano wa wenzao ambao wameshinda kwa kucheza na kuingia kwenye droo ili na wao washinde.

"Ninapenda kuwahamasisha Watanzania wenzangu husususani wateja wetu wa Vodacom kuchangamkia fursa hii. Mmoja wa washindi wa leo (jana) Charles Joseph ameshinda milioni moja hivyo basi iwe chachu kwa wengine kushiriki kadiri wawezavyo.

Kuweka pesa SportPesa kupitia M-Pesa, ingia kwenye menyu ya malipo ya M-Pesa kisha chagua lipa bili, halafu michezo, kisha SportPesa, halafu fuata maelezo.

Naye Meneja biashara kutoka Airtel, Aggrey Charles alisema wateja wa Airtel wajitahidi kucheza ili kushinda zawadi hizi za Bet Bonanza kama ambavyo mshindi Masoud Abdallah wa Mkuranga alivyoshinda milioni moja.

"Hii ni wiki ya pili na ninayofuraha kuona mshindi wa milioni moja kutoka Airtel amepatikana. Hii sio hela ndogo hivyo nawaasa wateja wetu waendelee kucheza na Sportpesa ili washinde zawadi hizi za Bet Bonanza.

"Nawasisitiza wateja wetu wajisajili na Sportpesa kisha waweke pesa kwa Airtel Money au kwa kutumia app yetu na baada ya hapo utaingia kwenye droo za kila siku na wiki kama hii ya leo ya milioni 1".

Kwa wale ambao hawakushinda wasikate tamaa kwani promosheni bado inaendelea kila siku hivyo waendelee kucheza.

Ikumbukwe promosheni hii ilizinduliwa rasmi siku ya tarehe 8 Machi ya wiki iliyopita inajumuisha zawadi za shilingi elfu 20 kila siku, zawadi za milioni moja moja kwa washindi watatu kila wiki na zawadi ya milioni 15,888,000 siku ya kufunga kampeni.




Baadhi ya mabalozi wa Sportpesa (Meena Ally, MC Gara B na Frank Charles Gibebe) walioshiriki kwenye droo ya pili ya promosheni ya Bet Bonanza wiki hii. Kushoto ni Meneja Mauzo Biashara- Mpesa, Kelvin Nyanda na wa pili kulia ni Meneja Mauzo Airtel Money- Biashara, Aggrey Charles. Washindi watatu wa Sh 1,000,000 kutoka mitandao ya Airtel, Vodacom na Halotel walitangazwa baada ya droo. **PICHA: SPORTPESA**

# Ligi Z'bar kusimama Mwezi Mtukufu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KLABU 16 za Ligi kuu ya Zanzibar zimekubaliana kwa pamoja michezo mitano ya ligi hiyo ichezwe mara baada ya kumalizika mwezi Mtukufu wa Ramadhani unaotarajiwa kuanza Aprili.

Makubaliano hayo yamefikiwa katika kikao cha pamoja kilichokutanisha viongozi wa Klabu hizo pamoja na viongozi wa Bodi ya Ligi Zanzibar.

Ligi Kuu ya Zanzibar wiki hii inaendelea na mzunguko wa 24 , kwa makubaliano hayo timu zitacheza michezo 25 huku michezo mitano itaendelea kuchezwa Mei 13 , baada ya kukamilika Mwezi wa Ramadhani.

Ligi hiyo inakwenda katika mapumziko mafupi kupisha ibada ya funga huku ikiwa bado bingwa wa ligi hiyo hajajulikana, lakini baadhi ya wadau wa Soka Visiwani hapa wanaendeleza kumpa nafasi kubwa KMKM huwenda akawa Bingwa Msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashimu Salum alisema ligi hiyo itaendelea mapema Mei kwa mfumo ule ule.

Alisema klabu zote 16 zilitoa maoni yao hayo na hadi kufikia hatua ya kusimama kwa muda mfupi kulingana na mazingira na tamaduni za Zanzibar husussani kwa mwezi wa Ramadhani.

# Michezo

Ijumaa Machi 25, 2022

Nipashe




Origi kutimka Liverpool UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini kujiandaa na mchezo wa mwisho wa makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Us Gendarmarie utakaopigwa Aprili 3, mwaka huu. **PICHA SIMBA**

# Simba yajipanga robo fainali CAF

## ●●● Yaweka mikakati kuhakikisha Gendarmarie hawatoboi kwa Mkapa na...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umeweka mikakati mizito kuhakikisha wanashinda mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi na kucheza robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu.

**Simba inatarajiwa kushuka dimbani Aprili 3, mwaka huu, wakiwakaribisha Us Gendarmarie katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesisitiza kutumia vema uwanja wa nyumbani kuhakikisha wanaibuka na ushindi.

Alisema wanahitaji ushindi wowote dhidi ya Gendarmarie katika mchezo wao wa mwisho ili kufuzu robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika bila kujali matokeo ya mechi ya RS Berkane dhidi ya Asec Mimosas.

"Tunapeleka maombi Shirikisho la Soka Afrika, CAF, ya kuruhusu idadi kubwa zaidi ya mashabiki, tumepoteza mchezo uliopita lakini hatujapoteza lengo la kutinga robo fainali," alisema Ally.

Tiketi yetu ya kutinga robo fainali tunayo wenyewe, tunahitaji kushinda tu mchezo wetu bila kuangalia matokeo ya mechi nyingine ndio maana nasisitiza mashabiki kujitokeza kwa wingi Aprili 3 kwa kusapoti timu."

Alisema mipango yao ilikuwa kuweka rekodi ya kutinga robo fainali ugenini, lakini hawakufanikiwa na sasa wameweka mipango sawa kuhakikisha katika dimba la Mkapa wapinzani wao hawatoki.

Alisema kabla ya kurudi nchini na wachezaji wengine kwenda katika majukumu ya timu za Taifa, viongozi walikutana nao na kukubaliana mechi ya mwisho watapambana hadi jasho la mwisho dhidi ya Gendarmerie ili kutafuta matokeo ya kwenda kucheza robo fainali.

## Fowadi yamkuna Poulsen

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa, 'Taifa Stars', Kim Poulsen, amefurahishwa na safu ya ushambuliaji walivyocheza na kukiri bado ana kazi kubwa ya kufanya kwa mabeki wake.

Stars juzi walipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati katika mchezo wa kirafiki ambao upo kwenye kalenda ya Shirikisho la Soka la Kimataifa, FIFA.

Mabao ya Stars yalifungwa na Novatus Dismas dakika ya 9 kwa shuti la adhabu ndogo baada ya kiungo Feisal Salum kuchezewa faulo na golikipa.

Bao la pili limefungwa na Mbwana Samata dakika ya 61 kwa pasi ya Farid Mussa ambaye aliingia kipindi cha pili huku, George Mpole aliyetokea benchi akipachika la tatu dakika ya 90 na bao la Jamhuri ya Kati lilifungwa na Yawanendji Theodore kwa mkwaju wa penalti.

Akizungumza na gazeti hili jana, Poulsen alisema ameridhishwa na kiwango kizuri kilichooneshwa na wachezaji wake hasa safu ya ushambuliaji kucheza kwa ubora wa hali ya juu.

Alisema wamepata mabao 3-1 na kutengeneza nafasi nyingi za mabao na kwamba anaridhishwa na kuona kwa mara ya kwanza safu hiyo ikicheza vizuri zaidi na utulivu mkubwa.

"Nimeridhishwa na kiwango cha timu, zaidi nimefurahishwa na bao la pili lilivyofungwa, nina imani mchanganyiko wa wachezaji utasaidia kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu ikiwemo AFCON na CHAN," alisema Poulsen.

"Bado tuna kazi kubwa kwenye safu ya ulinzi kwa sababu kuna muda wanajisahau na kupoteza umakini, hili jambo nafikiria sio zuri hasa unapokutana na mpinzani mzuri."

Alisema kuhusu sura mpya aliowaita hasa wale wanaocheza soka la kulipwa kama Haji Mnogas, Ben Starkie na Adi Yusuph kutocheza vizuri sana ni kutokana na kutozoea mazingira (hali ya hewa kwa haraka).


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >